

## YANGA SC YATAKATA CAF

UKURASA 24

## HAWARA mbaroni tuhuma kuchoma nyumba na kuua

UKURASA 4



## UCHAGUZI DRC: Katumbi ajigamba kushinda, Fayulu

UKURASA 19


# Nipashe

Alhamisi Desemba 21, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581531

www.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper


### LICHA YA MVUA KUBWA...

# Kilichojificha mgawo wa umeme TANESCO

UKURASA 2



Filichesmi Mramba

## NIDA yatoa siku 14 kwa wananchi kufuata kadi zao serikali za mitaa

UKURASA 2




UKURASA WA 4

## MAHAKAMA KUU YAINGILIA KATI MGOGORO WA UMILIKI WA SHULE

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Bukoba, imeingilia kati mgogoro wa umiliki wa Shule ya Sekondari Jipe Moyo iliyoko katika Kata ya Ngenge, Muleba

# Dawa bandia zanaswa mikoa 13

UKURASA 3

MICHEZO BENCHIKHA: BADO HATUJAMALIZA KAZI UK. 24 KATUNI UK. 6



Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara, Maryam Muhaji na Katibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria, George Nathaniel Mandepo wakiapa kiapo cha maadili katika hafla iliyofanyika Ikulu Jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Kilichojificha mgawo wa umeme

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Nishati, Felchesmi Mramba, amesema mgawo wa umeme unaoendelea hivi sasa katika maeneo mengi ya nchi, utakwisha kuanzia wiki ya tatu ya mwezi Januari mwakani.

Mramba alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kukagua kiwango cha maji katika chanzo cha kuzalisha umeme cha Bwawa la Mtera.

"Hivi sasa kweli hali ni mbaya ya umeme nchini kutokana na vyanzo vyetu tunavyovitegemea kuzalisha umeme, kikiwamo hiki cha Mtera, kukosa maji licha ya kuwapo mvua katika maeneo mbalimbali ya nchi.

"Lakini mvua hii ambayo inanyesha hivi sasa, ni kwa mikoa ya Kanda ya Pwani na Ziwa Victoria, hivyo vyanzo vyetu vya Mtera na Kidatu havipati maji ya mvua hii," alisema.

Mramba alisema kuwa kutokana mvua ambayo inatarajiwa kuanza kunyesha kati ya Desemba 25 na 26 mwaka huu, maji yataongezeka katika vyanzo hivyo ambavyo vinategemea maji kutoka mikoa ya Iringa, Mbeya, Tabora, Singida na Dodoma.

"Lakini pia mtambo wa kwanza wa kuzalisha umeme katika Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere utaanza majaribio Januari 16, 2024 ambao utaongeza Megawati 235 kwenye Gridi ya Taifa na kuongeza kiasi cha umeme," alisema.

Kadhalika, alisema mtambo wa pili utaanza majaribio mwezi Machi na kuongeza Megawati zingine 235 na kufanya mgawo wa umeme kuisha kabisa nchini.

"Niwahakikishie watanzania, kweli hivi sasa tuna njaa lakini chakula kipo jirani kabisa kwani katika kipindi hiki kuanzia wiki ya tatu ya mwezi Januari 2024 hadi mwezi Machi tatizo la mgawo litakuwa limekwisha kabisa nchini," alisema.

Alisema pamoja na kusubiri mvua kuanza kunyesha na majaribio ya mitambo ya kuzalisha umeme katika Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere, wanaendelea na jitihada za kufanyia kazi malalamiko ikiwamo kupunguza makali ya umeme.

"Hivi sasa kuna malalamiko mengi kwa wananchi kuhusu mgawo mkali wa umeme katika baadhi ya maeneo na maeneo mengine kupendelewa," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme (TANESCO), Gissima Nyamo-Hanga, alisema mgawo wa umeme unaoendelea unazingatia mahitaji na kusisitiza kuwa shirika lake limekuwa linasimamia kwa umakini mgawo huo.

"Mkakati wetu ni kuhakikisha mgawo unakuwa si wa kuuliza na umeme unarejeshwa kwenye maeneo ya mgawo kwa muda uliopangwa," alisema.

Nyamo-Hanga pia alisema mvua inayonyesha ukanda wa Pwani na ziwa haitoi majibu katika kuzalisha umeme katika vituo vya Mtera na Kidatu.

"Mvua za Pwani zinapeleka maji Bahari ya Hindi na vituo vya Mtera na Kidatu vinategemea mvua ambayo inanyesha mikoa ya Iringa na Mbeya inayojaza mito ya Ruaha Mkuu na Ruaha Mdogo wakati Mto Kizigo unajanzwa na mvua za Tabora, Singida na Dodoma.

Kaimu Mkurugenzi wa Uzalishaji TANESCO, Aloyce Simon alisema kwa sasa Bwawa la Mtera linazalisha megawati 40 chini ya uwezo wake wa kuzalisha megawati 80, yaani linazalisha nusu ya uwezo wake.

"Maji haya yakizalisha umeme hapa yanakwenda kuzalisha umeme katika kituo chetu cha Kidatu, hivyo kutokana na hali ya maji kuwa kina cha chini, linazalisha megawati 40 yanakwenda Kidatu na kuzalisha megawati 60 chini ya uwezo wa kituo hicho ya kuzalisha megawati 200," alibainisha.

Awali Kaimu Meneja wa Kituo cha Kufua Umeme cha Mtera, Moses Holela, alisema kuwa baada ya mvua kidogo kunyenya Kanda ya Kati, bwawa limefikia kina cha chini cha mita za ujazo 690.4 juu ya usawa wa bahari ambapo kiwango cha wastani ni mita za ujazo 698.5 juu ya usawa wa bahari.

## NIDA yatoa siku 14 wananchi kufuata vitambulisho

**Na Jenifer Gilla**

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), imetoa siku 14 kwa wananchi waliojiandikisha kwenda kuchukua vitambulisho katika ofisi za serikali ya mtaa, vijiji au vitongoji katika maeneo wanayoishi.

Kwa mujibu wa NIDA, baada ya hapo watalazimika kuvifuata katika ofisi za wilaya katika mikoa yao.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa NIDA, Geoffrey Tengeneza, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika ufunguzi wa mafunzo kwa waandishi wa habari kuhusu namna ya kuripoti matukio ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na uhalifu yaliyoandaliwa na mamlaka hiyo kwa kushirikiana na wizara.

Alisema ugawaji wa vitambulisho hivyo kwa awamu hii, utahusisha wananchi walioko katika mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Dodoma, Arusha, Morogoro, Mbeya na Ruvuma. Aliwasisitiza watu wa maeneo hayo kutumia fursa hiyo vizuri ili kuepuka usumbufu wa kuvifuata mbali.

Tengeneza alisema lengo la kuanzisha utaratibu huo ni kumrahisishia mwananchi mchakato wa kupata kitambulisho, kuhakikisha kila mwananchi aliyejiandikisha anakipata kwa haraka na kusiwapo na vitambulisho vitakavyobaki katika ofisi ya serikali ya mtaa au kijiji kama ilivyokuwa awali.

"Kwa hiyo wananchi watumie fursa hii wakachukue vitambulisho kule. Muda wa siku 14 ukiisha tutavikusanya vitambulisho vyote vilivyosalia na kuvirudisha katika ofisi zetu za usajili za wilaya. Mwananchi ambaye hatakwenda kwa muda huo, atalazimika kukifuata kwenye ofisi ya NIDA ya wilaya alikojisajili," alisema.

Alisema awamu hii NIDA imezalisha vitambulisho milioni 14 na tayari vile vya mikoani vimeshapelekwa hadi vijijini na vitagawiwa kwa watu wenye namba za utambulisho na kwamba malengo mpaka kufikia Machi, mwakani, kila Mtanzania awe na kitambulisho chake.

Tengeneza alisema kwa ujumla mpaka sasa wameshatoa namba za utambulisho (NAN) milioni 20.7 katika hao wamechapisha vitambulisho milioni 18.7 sawa na takribani asilimia 90 ya vitambulisho vinavyohitajika.

Akifungua mafunzo hayo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Kaspar Mmuya, aliwaelekeza waandishi wa habari hasa za mitandaoni wanapoandika habari zinazohusiana na wizara hiyo, kuzingatia weledi ili kuepuka kuzua hofu, taharuki, kuleta vurugu, uchochezi au kuondoa amani na utulivu uliopo nchini.

Alisema baadhi ya mitandao ya kijamii imekuwa ikiripoti habari za matukio ya kihalifu, majanga yanayohitaji uokozi pasipo kuzingatia taaluma au miiko ya uandishi wa habari na matokeo yake kusababisha uhasama, uadui, chuki na visasi katika jamii.

"Kutokana na kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano hivi sasa kumeibuka tabia ya kila mtu kutaka kuandika na kusambaza habari kupitia mitandao ya kijamii na "platform" mbalimbali bila kujua madhara ya habari inayoandikwa ni yapi kwa mtu mmoja mmoja, kwa familia na taifa kwa ujumla," alisema.

Mmuya alisema wizara hiyo ina jukumu kubwa la kusimamia usalama wa raia na mali zao na kuhakikisha nchi hiyo inakuwa na amani na utulivu.

Alisema wizara iliona changamoto hiyo kwa waandishi wa Habari, hivyo ikaamua kuandaa mafunzo namna ya kuripoti matukio hayo kwa kuzingatia sheria za nchi, maadili ya uandishi wa habari na weledi ili kwa pamoja wawe walinzi wa raia na mali zao.

# Wamiliki wa malori walia na polisi

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Wamiliki wa Malori Tanzania (TAMSTOA) kimeliomba Jeshi la Polisi nchini litoe elimu kwa watendaji wake wa usalama barabarani ili wapunguze kukamata malori yanayosafirisha mizigo kwenda nje ya nchi.

Mwenyekiti wa chama hicho, Chuki Shaban, alitoa rai hiyo wakati wa mkutano mkuu wa nne wa mwaka wa chama hicho uliofanyika Dar es Salaam juzi.

Alisema, "zipo kamatakamata za hapa na pale ambazo baadhi ya watendaji wa barabarani wa jeshi hilo wamekuwa wakifanya barabarani kwa malori yanayopeleka mizigo nje ya nchi."

Alisema jambo hilo limekuwa linachelewesha kufikisha mizigo kwa wakati katika nchi inakopelekwa.

Pia alisema kucheleweshwa kwa malori barabarani kunarudisha nyuma maendele ambayo serikali inapambana kuyainua kupitia sekta ya uchukuzi.

"Mambo mengi yalikuwa yanatukumba kwenye sekta hii ya usafirishaji, lakini serikali yetu ni sikivu ikayatatua. Sasa hivi kuna vitu vidogovidogo ambavyo tunaamini navyo vitatatuliwa.

"Kwa mfano, hivi karibuni nilipita Kibaha mkoani Pwani, nikakuta malori matano yamekaa pale kwa saa nne, wanasema wanadaiwa Sh. 50,000 ambayo waliandikiwa na trafiki wa usalama barabarani.

"Yaani mtu anasafiri masafa marefu halafu unamweka hapo muda wote huo, hilo gari si linakwenda na linarudi, kwanini asiruhusiwe awahishe mzigo kwanza? Kwahiyo, tunachoomba Jeshi la Polisi lijitahidi kuwapa elimu watendaji wake," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa mara nyingi serikali imeonesha nia njema kwao kwa kuwa mstari wa mbele kutatua changamoto kubwa ambazo hujitokeza na waanamini hata hayo madogo yaliyobaki yatatatuliwa.

"Serikali inajitahidi kutatua changamoto zetu kwa wakati, linapojitokeza jambo tukienda kuwalilia tunakaa pamoja tunalimaliza. Kwa kifupi, ni kwamba serikali yetu ni sikivu kwa mambo yetu mengi," alisema Shaban.

Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Barabarani kutoka Wizara ya Uchukuzi, Andrew Magombana, alisema serikali iko pamoja na wasafirishaji wa malori hususani katika kuwawekea mazingira mazuri ya kufanyia biashara na kutatua changamoto zao.

"Serikali iko pamoja na wasafirishaji wa malori, tunasikiliza changamoto zao zote, tunawafungulia mikataba yao na nchi jirani, kuhakikisha uwekezaji wao unarudi katika fedha walizowekeza," alisema Magombana.

# TMDA yakamata dawa bandia mikoa 13

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), imekamata dawa zisizosajiliwa zenye thamani ya Sh. milioni 133.3 katika mikoa 13 kupitia operesheni maalum ya kukamata dawa, vifaa tiba na vitendanishi vya serikali, bandia, duni, zisizo na usajili na dawa za kulevya iliyofanyika mwezi uliopita.

Vilevile, faini za Sh. milioni 100 zikusanywa kutokana na makosa hayo na majalada 13 yamefunguliwa dhidi ya watuhumiwa wakati taratibu za kuwafikisha mahakamani zinaendelea.

Mkurugenzi Mtendaji wa TMDA, Adam Fimbo, alibainisha hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuhusu operesheni hiyo iliyofanyika kuanzia Novemba 20 hadi 24 mwaka huu.

Alisema operesheni hiyo ilihusisha pia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kilevya (DCEA), Baraza la Famasia Tanzania, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa ma Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Jeshi la Polisi katika mikoa ya Dar es Saam, Dodoma, Morogoro, Kigoma, Katavi, Mwanza, Simiyu, Arusha, Kilimanjaro, Mbeya, Songwe, Lindi na Ruvuma.

Alisema pia walikamata vifaa tiba na vitendanishi ambavyo havijasajiliwa na kutambuliwa vyenye thamani ya Sh. milioni 17.7 katika kanda zote.

Fimbo alisema pia walikamata dawa zenye madhara ya kulevya aina ya Pethidine kwenye maeneo mbalimbali zikiuzwa kwa siri na mtandao wote ulibainika na wahusika kufahamika.

Alisema pia wamekamata vifaa tiba vilivyoisha muda wa matumizi vyenye thamani inayokadiriwa kuwa vya Sh. milioni 10.3 vikiwa havijatengwa kwa mujibu wa taratibu.

Fimbo alisema walikamata dawa bandia za binadamu zenye thamani ya Sh. milioni 5.9 katika Kanda ya Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini na Magharibi.

"Dawa zote bandia zilizokamatwa zilikuwa ni za mifugo ambazo ni Bupanor Injection, Homidium Chloride 250mg BP, Homidum Chloride 250mg, Ehithidium Bromide, Samocare (Isometamidium Chloride Hydrochloride Ig), Bromidium na Veridum Ig (Isometamedium Chloride Hydrochloride)," alibainisha. Fimbo pia alisema dawa zenye ubora duni za thamani ya Sh. 579,600 zilikamatwa Kanda ya Kaskazini, Mashariki na Kati.

Alizitaja dawa hizo kuwa ni U-sol (Chlorinated lime and Baric Acid), dawa za mifugo aina ya Bamisole 10% (Levamisole Injection) ambayo ilikutwa imebadilika rangi kutoka njano na kuwa nyeupe kama maji na Ibefun 200.

Fimbo alisema walikuta vifaa na vitendanishi duni vyenye thamani ya Sh. 5.4. Vilikamatwa Kanda ya Ziwa na Kanda ya Mashariki.

Sambamba hilo, alisema sehemu za biashara za majengo 777 yaliyokaguliwa, walibaini majengo 200 yalikutwa na dawa zisizosajiliwa na kutambuliwa.

Alisema pia majengo 125 yalikutwa na bidhaa zilizoisha muda wa matumizi ambazo hazikuwa zimetengwa.

Majengo mengine 84 hayakuwa na vibali vya biashara, 67 hayakuwa na wataalamu, 66 hayakuwa na nyaraka za ununuzi, 64 yalikutwa na dawa zisizoruhusiwa kuwapo katika DLDM na 36 yalikuwa na bidhaa za serikali.

"Huu ni mwendelezo wa operesheni zetu katika kuhakikisha tunalinda afya ya mlaji na udhibiti wa matumizi ya dawa bandia na zilizoisha muda wake ha bidhaa zote tulizokutwa na kasoro zilionдolewa sokoni kwa maslahi ya watumiaji ili kuondokana na madhara," alisisitiza Fimbo.

Msajili wa Baraza la Famasia Tanzania, Elizabeth Shekalaghe, alisema wanataaluma waliokutwa kwenye maeneo yao na makosa mbalimbali watachukuliwa hatua za kisheria.

Alisema wamiliki wote wa dawa wanatakiwa kununua katika maeneo rasmi yaliyosajiliwa kwa sababu kununua mikononi ni kuvunja sheria na taratibu za usajili.

Vilevile, alionya wamiliki wa maduka ya dawa wanaotoa huduma za vipimo vya magonjwa kama malaria na mkojo (UTI) kinyume cha taratibu za utoaji huduma za afya nchini.


## KUPOTEA KWA CHETI CHA USAJILI

**THE SOCIETY OF ST. VICENT DE PAUL IN TANZANIA**
inatangaza kupotea kwa Cheti cha usajili chenye namba **5509** kilichotolewa na RITA. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/ARU/9609/2023.**

## KIBAIGWA AUCTION MART
**P.O.BOX 20, DODOMA**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**KIBAIGWA AUCTION MART,** KWA IDHINI NILIYOPEWA NA KAMPUNI YA IMARISHA MAISHA FINANCIAL SERVICES LTD. TUTAUZA GARI MOJA MALI YA JACKSON RYOBA KANGOYE YENYE NAMBA ZA USAJILI T 439 DMU AINA YA NISSAN ELGRAND . BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIOKOPA. MNADA UTAFANYIKA TAREHE 22/01/2024 MAENEO YA NYERERE SQUARE SAA 10:00 ASUBUHI

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NO. 0688 729841**

## The Guardian Limited

## VACANCY

### Freelancer Sales Executive

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales personnel to join our **advertising** Sales Team in **Dar es Salaam, Arusha and Zanzibar**

**Responsibilities**

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

**Qualifications**

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

**NOTE: This is a commission Based Position**

**Please send your application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 28th December, 2023.**

HABARI KITAIFA

# Mahakama Kuu yaingilia kati mgogoro wa umiliki wa shule

**Na Jenesta Jasson,** MULEBA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Bukoba, imeingilia kati mgogoro wa umiliki wa Shule ya Sekondari Jipe Moyo iliyoko katika Kata ya Ngenge, Muleba baada ya kukubali maombi ya zuio la kukabidhiwa kwa mmiliki mwingine.

Shule hiyo inayomilikiwa na Mmosinyoli wa Kanisa Katoliki, Dk. Gozibert Byamungu, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Muleba ilihitaji kuikabidhi katika umiliki wa Haruna Mfunda anayedai kuinunua mtu aliyetajwa kwa jina la Mukurasi ambaye kwa sasa ni marehemu.

Akiwasilisha maombi ya kuzuia hatua hiyo mbele ya Jaji Ayoub Mwenda, Wakili wa Dk. Byamungu, Prosper Mulokozi, alisema hatua ya kukabidhi shule hiyo kwa Mfunda iliyokuwa itekelezwe na Mkuu wa Wilaya ya Muleba, Dk. Abel Nyamahanga, inatakiwa kusikilizwa mbele ya mahakama hiyo kabla ya kutekelezwa.

Wakili Mulokozi aliwasilisha pia na mapingamizi mengine ikiwamo hatua ya mkuu wa wilaya kuwafukuza watumishi wote katika mazingira ya shule wakiwamo walimu na kuweka ulinzi wa kuwazuia watumishi hao kukanyaga shuleni hapo.

Alidai kuwa mteja wake hakutendewa haki, hivyo kupitia uamuzi wa mahakama hiyo, watapata haki na uamuzi sahihi katika kushughulikia mgogoro wa pande mbili zinazopingana.

Baada ya kusikiliza maombi hayo, Jaji Mwenda alisema alipokea na kuita pande zote mbili za mgogoro kuhudhuria mahakamani kesho ili wote wasikilizwe na kutolewa uamuzi wa haki kwa pande zote.

Akizungumza nje ya Mahakama hiyo, Wakili Mulokozi alisema tayari ametoa notisi ya siku 90 kwa serikali kupinga vitendo alivyofanyiwa mteja wake.

Alisema baada ya siku 90 kama serikali haitajibu hoja za kulalamikiwa, atafungua kesi mahakamani itakayomhusisha Dk. Nyamahanga kama yeye binafsi kwa sababu ya kutoa agizo kumwondoa mteja wake kwenye shule anayoimiliki kihalali.



Ofisa Uhusiano wa kampuni ya Grumeti Fund ya wilayani Serengeti mkoani Mara, Domina Mgelwa (kushoto) akitoa maelezo kwa viongozi wa Hifadhi ya Jamii ya Wanyamapori ya Burunge (WMA) na wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara, jinsi uzio wa umeme ilivyosaidia baadhi ya vijiji vya Serengeti kudhibiti wanyamapori wakali wanaoharibu mazao, wakati wa ziara ya mafunzo kwenye WMA ya Ikona juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



## Serikali yamlilia Amir wa Kuwait

**Na Halfani Chusi**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mbarouk Nassor, ametia Saini kitabu cha maombolezo katika Ubalozi wa Kuwait jijini Dar es Salaam, kutokana na kifo cha Amir wa Kuwait, Sheikh Nawaf al-Ahmad Al-Sabah.

Kiongozi huyo alifariki dunia Desemba 16, mwaka huu, akiwa na umri wa miaka 86 baada ya kuliongoza taifa hilo kwa miaka mitatu.

Balozi Mbarouk alitoa salamu za pole kwa niaba ya serikali akisema kiongozi huyo atakumbukwa kama mwanadiplomasia na kiongozi imara aliyejitolea maisha yake katika masuala ya amani.

"Amir Sheik Al-Sabah atakumbukwa kama kiongozi mahiri wa Kuwait aliyeimarisha ushirikiano wa karibu kati ya nchi yake na Tanzania.

"Kwa niaba ya serikali, tunapenda kutoa salamu zetu za pole kwa wananchi wa Kuwait kwa kuondokewa na kiongozi bora na mpenda amani. Roho yake ipumzike mahali pema peponi," alisema Balozi Mbarouk

**"Amir Sheik Al-Sabah atakumbukwa kama kiongozi mahiri wa Kuwait aliyeimarisha ushirikiano wa karibu kati ya nchi yake na Tanzania.**

# Watatu mbaroni kwa tuhuma za mauaji

**Na Thomas Wandiba** SAUT

JESHI la Polisi mkoani Mwanza linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za mauaji ya Frola Philimoni, mfanyabiashara na mkazi wa Mtaa wa Kashishi Kata ya Nyamhongolo pamoja na hawara anayetuhumiwa kuchoma nyumba na kusababisha vifo vya watu watatu hivi karibuni.

Taarifa ya kukamatwa kwa watu hao ilitolewa jana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Wilibroad Mutafungwa.

Kamanda Mutafungwa aliwataja waliokamatwa kupitia uchunguzi uliofanywa na jeshi hilo kuwa ni Elizabeth Joseph (35) ambaye ni ndugu wa marehemu, mkazi wa Dar es Salaam na Faida Daudi (24) fundi wa Nyumba na Mkazi wa Igoma jijini Mwanza.

Alisema chanzo cha mauaji hayo ni migogoro ya kifamilia ya kugombania mali uliosababisha hivyo kusababisha mama huyo kuuawa kwa kukabwa shingo kisha kukatwa na kitu chenye ncha kali Novemba 11, mwaka huu.

"Uchunguzi wetu umebaini kuwa Elizabeth ambaye ni ndugu wa marehemu, walipanga njama na fundi huyo aliyekuwa akipaka lipu katika nyumba hiyo na kutekeleza mauaji hayo," alisema Mutafungwa

Katika hatua nyingine, Kamanda Mutafungwa alisema jeshi hilo limemkamata Nestory John (52) mkazi wa Buhongwa jijini Mwanza, hawara anayetuhumiwa kuhusika kuchoma nyumba moto na kusababisha vifo vya watu watatu (mama na watoto wawili) hivi karibuni.

"Baada ya msako mkali tulimkuta mtuhumiwa huyu mkoani Geita kwa mganga wa kienyeji, Samson Mwinamila (35), mkazi wa Sulagulwa akiwa anamfanyia dawa ili asikamatwe na polisi. Mganga huyo naye tumemkamata ili ajibu tuhuma za kuficha wahalifu," alisema SACP Mutafungwa

John anatuhumiwa kuchoma nyumba ya aliyekuwa hawara wake, Eva Stephano, Desemba 7, mwaka huu katika mtaa wa Lwanhima, Buhongwa, Nyamaga jijini Mwanza.

Moto huo ulisababisha vifo vya Stephano na Watoto wake wawili huku chanzo kikitajwa kuwa ni mgogoro wa mapenzi.

## Chuo Utumishi wa Umma chaja na mtaala mpya kwa watumishi

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

CHUO cha Utumishi wa Umma Tanzania kiko katika mchakato wa kuandaa mtaala mpya wa masomo unaolenga kuwapitisha watumishi wa umma katika ngazi mbalimbali za mafunzo kuanzia wanapoajiriwa hadi watakapostaafu.

Kaimu Mkuu wa Chuo, Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaaalamu wa chuo hicho, Dk. Hamisi Amani alibainisha hayo jana wakati wa mafunzo ya awali kwa watumishi wa umma 191 wa ajira mpya wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijni (RUWASA) yanayofanyika kwa siku nne katika ukumbi wa mikutano wa Bodi ya Bonde la Kati mjini Singida.

Alisema chuo hicho kimeshaona umuhimu wa kutoa mafunzo ya aina mbalimbali kwa watumishi wa umma na kipo katika mchakato wa kuandaa mtaala huo. Sasa kiko katika hatua mbalimbali za mamlaka ambazo zinatakiwa kupitisha mchakato huo.

Kwa mujibu wa Kaimu Mkuu wa chuo huyo, mazingira ya chuo yalivyo sasa, watumishi wengi wa serikali wanakuwa wanaingia katika ngazi mbalimbali baada ya kuteuliwa, lakini hawayajui majukumu mapya katika ngazi hizo na wanatakiwa wafanye vipi ili kuendana na majukumu yao mapya.

"Tuko hapa Singida leo (jana) kwa ajili ya ufunguzi wa mafunzo ya awali elekezi kwa watumishi wapya wa RUWASA ambao wapo watumishi takribani 191.

"Watumishi hawa wapya wanapatiwa mafunzo haya elekezi ya awali kwa sababu kwa upande wa serikali na taasisi zake, mafunzo elekezi kwa watumishi wapya katika taasisi hizo yanapaswa yatolewe na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania na hii ni kwa mujibu wa Waraka wa Utumishi Na. 5 wa Mwaka 2011," alisema.

Awali akifungua mafunzo hayo ya siku nne, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa RUWASHA, Bwai Biseko alitumia fursa hiyo kuwataka watumishi hao kujifunza zaidi na kuelewa vizuri taasisi yao.

"Bado mnahitaji kujifunza na kuielewa vizuri taasisi yenu, kuelewa vizuri utumishi wa umma na ili kuutumikia kwa mafanikio," alisema.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo walipongeza serikali kwa kuwaandalia mafunzo hayo kwa kuwa yatawasaidia kufahamu majukumu yao, miiko ya kazi na miongozo ya kiutumishi.

# TANROADS yatoa mbinu za kukabili mabadiliko tabianchi

**Na Christina Haule,** MOROGORO

KATIKA kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha madhara mengi, jamii inapaswa kufanya shughuli za kibinadamu kitaalamu ili madhara hayo yanayojumuisha uharibifu wa miundombinu na maafa katika baadhi ya maeneo.

Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Morogoro, Alinanuswe Kyamba, alitoa rai hiyo juzi alipozungumza na waandishi wa habari mjini hapa. Alisema mvua inayoendelea kunyesha kwa sasa inaonekana kuongezeka kutokana na shughuli za kibinadamu kufanyika bila kufuata taratibu za uhifadhi wa mazingira hasa jirani na vyanzo vya maji.

Kyamba alisema licha ya mvua hiyo kuendelea kunyesha, barabara zote katika Mkoa wa Morogoro zinapitika vizuri kwa sasa baada ya TANROADS kufanya marekebisho katika maeneo manne yaliyoharibika na kukata mawasiliano kwa saa mbili wenye wilaya za Kilosa na Morogoro.

Aliyataja maeneo yaliyopata athari za mvua hiyo ni barabara ya Dumila-Kilosa ambayo ilirekebishwa na makandarasi wazawa, wakitumia kampuni ya Kilosa JV inayotekeleza mradi wa barabara ya Ludewa-Kilosa yenye urefu wa Km 24.

Alisema ukarabati wa barabara hiyo umeshakamilika na wameshaikabidhi TANROADS na kubakiwa na ujenzi wa madaraja matatu ya Kobe, Mazinyungu na Ilonga.

Meneja huyop alisema mvua hiyo imeondoa michepuko kwenye madaraja ya Ilonga na Mazinyungu na kusababisha kukatika mawasiliano kwenye barabara ya Dumila-Kilosa. Sasa yamerejeshwa baada ya ukarabati wa siku mbili.

Kyamba aliitaja miundombinu mingine iliyoathirika kuwa ni daraja la Mto Mkondoa katika barabara ya Kilosa-Mikumi. Walifanya kazi ya marekebisho ndani ya siku mbili na kurejesha mawasiliano.

Alitaja eneo lingine lililoleta shida ni daraja la Dumila lililoko eneo la Mkundi ambako maji yalipita juu ya barabara na kukata kingo za daraja na baada ya maji kupungua, walimarisha kingo hizo.

Kyamba alitaja eneo lingine lililopata changamoto ni barabara ya Bigwa-Kisaki kwenye eneo la Mto Ruvu. Mkandarasi aliweka mawe ya kutosha na sasa kunapitika bila wasiwasi.

Aliwaomba wananchi kuwa na subira pale wanapoona mvua inanyesha na barabara ikiwa imefunikwa na maji, wasipite hadi watakapoona barabara ipo juu kuliko kukimbilia kuendelea na safari wakati barabara haionekani. Kunaweza kusababisha madhara makubwa ikiwamo vifo.

Mmoja wa wakazi wa Kilosa, wilayani Morogoro, Latifa Mihayo aliishukuru serikali kwa jitihada walizoonesha za kukamilisha ukarabati wa madaraja na barabara wilayani humo na kurejesha mawasiliano kwa muda mfupi baada ya kukatika.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Jenista Mhagama akipokea mchango wa Walimu Wakuu wa shule za Sekondari nchini kwa ajili ya waathirika wa maafa ya maporomoko ya matope na mawe kutoka mlima Hanang uliowasilishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI Mohamed Mchengerwa kwa niaba yao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijana 330 kunufaika mafunzo ujasiriamali, vifaa vya masomo

**Na Romana Mallya**

VIJANA 331 kati ya 1,732 walionufaika na mafunzo ya ujasiriamali, kujitambua na kujisimamia wamepatiwa vifaa vya shuleni, saluni na vyerehani kwa lengo la kujikwamua kiuchumi.

Vifaa hivyo vimetolewa chini ya mradi wa AIM (Accelerating Impact for Young Women) unaotekelezwa kwa miaka mitano nchini na Brac Maendeleo Tanzania kwa wasichana na wavulana wenye umri wa miaka 12 hadi 35.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Dar es Salaam, Given Sure, akizungumza jana katika hafla ya kukabidhi vifaa hivyo kwa wanufaika iliyofanyika Shule ya Msingi Buguruni jijini, aliwataka waliofuzu mafunzo hayo kuwa mabalozi.

Kati ya walionufaika, wapo waliopata ujauzito wakiwa shuleni ambao wamepatiwa vyerehani na vifaa vya saluni na wengine ni wanafunzi wanaoendelea na masomo.

"Mashirika yasiyo ya kiserikali yapo maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kuifikia jamii. Katika Jiji la Dar es Salaam, Brac walianzisha mradi huu ukilenga kata tatu, lakini zilizofuzu mafunzo ni mbili ambazo ni Buguruni na Vingunguti," alisema.

Alisema programu za aina hiyo husaidia kuinua jamii katika shughuli za kiuchumi kwa kuwa wanufaika wanapatiwa vifaa vya saluni na vyerehani.

Given aliwataka wanufaika wa mradi huo watakapokabidhiwa vifaa hivyo, wasiviuze bali wavitumie kujikwamua kiuchumi.

Pia aliwataka wanafunzi waliopewa vifaa vya shuleni ambavyo ni mabegi, madaftari na kalamu, kuhakikisha wanafanya vizuri katika masomo yao darasani na kuwa na maadili.

Desideri Mulagala, akizungumza kwa niaba ya Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, aliwakumbusha walezi na wazazi wa vijana na wanafunzi hao kuwa umri wa watoto wao ni sawa na moto wa kifuu, hivyo wahakikishe wanawalea ipasavyo.

"Mabinti na vijana mnaokwenda kutekeleza mradi kwa vitendo ninawaomba muone kilichofanyika ni cha msingi cha kuwaondoka katika umaskini.

"Mmejengewa uwezo wa kupata maarifa kwa miezi sita na mmejengewa uwezo kwa kukabidhiwa vifaa, mkafanye kazi iliyokusudiwa ili baada ya miezi sita, tathmini itakayofanyika ionyeshe wamefanikiwa kwa kiwango gani," alisema.

Meneja wa Tawi la Buguruni wa mradi huo, Caroline Buyamba, alisema mradi huo umetekelezwa ndani ya miezi sita katika kata hizo.

Alisema mwaka jana walipoanza kutekeleza mradi huo wa miaka mitano, walipata wavulana na mabinti 1,732 na kufungua klabu 12 ambapo kati ya hizo, sita zilifunguliwa Vingunguti, tatu Mnyamani na tatu Buguruni.

Alisema kigezo kimojawapo kwa wanufaika kilikuwa ni ushiriki wa darasani kwa asilimia 70 ambapo kati ya kata hizo, mbili ndizo zilizofuzu ambazo ni Buguruni na Vingunguti waliosoma kwa miezi sita.

Alisema miongoni mwa mambo waliyokuwa wanafundishwa ni kujitambua, kujisimamia na kuweza kuishi na watu wengine.

Alisema waliopatiwa vifaa vya shuleni ni 162, vyerehani ni 97 na washiriki 72 wamepatiwa vifaa vya saluni, hivyo kuwa na jumla kuu ya wanufaika 331.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ajali za mwisho wa mwaka zidhibitiwe kwa ukamilifu

**MSIMU** wa sikukuu za mwisho wa mwaka umewadia. Ni wakati ambao Watanzania na watu wengine duniani husherehekea sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya kwa kujumuika na ndugu na jamaa kula, kunywa na kubadilishana mawazo huku wanafamilia wakijaribu kufanya tathmini ya mwaka kupanga mambo ya kufanya kwa mwaka mpya.

Baadhi ya watu husafiri kwenda mapumziko nje ya sehemu wanazofanyia shughuli zao za kujipatia kipato, kwa maana ya ajira na biashara, husafiri kwenda ama sehemu walikozaliwa au wanazochagua kwenda kupumzika. Kwa sasa tayari baadhi ya familia zimeshasafiri kwenda sehemu walizochagua na wengine wako katika maandalizi ya kusafiri.

Kutokana na pilikapilika za sherehe hizo na mapumziko ya mwisho wa mwaka, kumekuwa na matukio mengi katika kipindi hiki zikiwamo ajali za barabarani ambazo hugharimu maisha ya watu na kuacha wengine wakipata ulemavu wa kudumu pamoja na uharibifu wa vyombo vya moto. Kuwapo kwa ajali hizo, kumeibua msemo kwamba hata shetani hutumia muda kama huo kuvuna.

Ni kweli kwa muda mrefu katika majira kama haya, zimeshuhudiwa ajali mbalimbali za mabasi na magari binafsi ambayo hutumika kwa ajili ya kusafiria watu kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Kama ilivyo ada, sababu kubwa ambazo zimekuwa zikitajwa ni uzembe wa madereva ikiwamo kutokuzingatia sheria za usalama barabarani na mwendokasi kwa baadhi ya wanaoendesha vyombo hivyo vya moto.

Sababu kama hizo zimekuwa zikitajwa kila mwaka kuwa ni chanzo cha watu kupoteza maisha mwishoni mwa mwaka wakati wakienda kwenye mapumziko au kurejea baada ya kumaliza mambo yao.

Pamoja na sababu hizo kutajwa na kuwa kama nyimbo midomoni mwa mamlaka, inashangaza kuona hakuna hatua zinazochukuliwa kudhibiti au kupunguza tatizo hilo. Kwa maneno mengine, sababu hizo ni kama hadithi ya alfu ulela ulela, kwa maana ya hadithi zisizo na mwisho.

Ni wazi kwamba kabla ya chombo chochote kuanza safari, hakina budi kukaguliwa ili kujiridhisha usalama wake. Kutokana na kuwapo kwa ajali kila mwaka, swali la kujiuliza ni je, ukaguzi huo umekuwa ukifanyika kwa umakini ili kuepuka kutokea kwa ajali za mara kwa mara? Na kama sababu ni mwendokasi, askari wa usalama barabarani wanatekeleza wajibu wao kuhakikisha hakuna dereva anayekwenda zaidi ya mwendo uliokubalika?

Kwa ujumla, suala hili limekuwa sugu kutokana na ukweli kwamba taarifa kuhusu kutokea kwa ajali za barabarani zimekuwa za kawaida miongoni mwa Watanzania hali inayoonyesha kuwa ni jambo la kawaida.


Umefika wakati sasa taasisi zilizopewa jukumu la kudhibiti ajali za barabarani ambazo zimekuwa zikigharimu maisha ya Watanzania, wengi wakiwa nguvu kazi inayotegemewa kwa maendeleo ya taifa, zizinduke na kuchukua hatua stahiki katika kudhibiti tatizo hili.

Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani, kwa mfano, linapaswa kuchukua hatua dhidi ya madereva wanaokiuka sheria za barabarani na baadhi ya magari binafsi yanayoonekana kuwa mabovu.

Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) inapaswa kutoa vibali kwa magari yanayokidhi viwango vya kusafirisha abiria na kuwapoka leseni wanaokiuka sheria.

Kama hayo yatafanyika, ni wazi kwamba ajali kama za mwisho wa mwaka ambazo zimekuwa zikisababisha madhara makubwa kwa binadamu na mali zitapungua na hata kuwa historia kwa taifa la Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Mary Seme

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kwa hili kuongeza vituo kujaza gesi, tuipongeze serikali, hatua inapigwa

**NOVEMBA** 11 mwaka huu, serikali ilizindua kituo cha kwanza cha kisasa cha kujaza gesi asilia kwenye magari (CNG) pamoja na karakana ya kufunga mfumo wa gesi hiyo ikiwa ni muendelezo wa kuchochea nishati safi na salama kwa mazingira.

Naibu Waziri Mkuu Dk.Doto Biteko aliyekuwa mgeni rasmi katika shughuli hiyo ya uzinduzi alisema serikali ipo katika jitihada za kuleta mabadiliko katika sekta ya nishati nchini. Jitihada hizi za serikali zinajibu kilio cha muda mrefu cha wale waliofunga mfumo wa gesi katika magari yao na wale wanaotamani kufanya hivyo.

Uchache wa vituo vya kujaza gesi, ndilo tatizo kuu kwa sasa kwa wale ambao tayari wamefunga mfumo huo katika vyombo vyao hivyo jitihada hizi ni za kupongezwa.

Pamekuwapo malalamiko ya foleni ndefu katika kituo cha kujaza gesi cha Ubungo Maziwa Dar es Salaam wakati wa kujaza gesi katika magari.

Gesi imeelezwa kuwa na bei nafuu, ikilinganishwa na mafuta kwamba kilo moja ya gesi ni Sh.1550 wakati ambapo lita moja ya petroli ni zaidi ya Sh.3000 kwa bei ya jijini Dar es Salaam.

Hivyo, mfumo wa gesi utasaidia kupunguza gharama za maisha kwa wananchi kwa kuwa usafiri na usafirishaji ni sekta inayomgusa kila mmoja.

Kama mtu hatatumia usafiri basi angalau atatumia bidhaa zilizosafirishwa na kwa hiyo gharama za usafirishaji zikiwa juu hata bidhaa za kutumia zinakuwa juu pia, hivyo kumuathiri hata yule asiyetumia usafiri mara kwa mara.

Mnamo Machi mwaka huu, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) liliahidi kujenga vituo vipya tisa vya kujaza gesi katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, ili kupunguza adha iliyopo ya foleni wakati wa kujaza gesi katika kituo cha Ubungo ndani ya miezi 24 kutokea wakati huo ambapo kwa sasa imeshapita miezi nane tangu kutolewa ahadi hiyo.

Tanzania inakadiriwa kuwa na mita trilioni 230 za ujazo za gesi asilia, ingawa zilizothibitishwa mpaka sasa ni futi trilioni 57.5. Taarifa zinaonyesha kuwa matumizi ya gesi ni nafuu kuliko petroli au dizeli, kwani hupunguza gharama kwa takriban asilimia 50.

Ninaamini kwamba, matumizi ya gesi yatakapokuwa katika kiwango cha juu nchini basi itakuwa ni neema kwa Watanzania kwa kuwa licha ya kuwa na hifadhi kubwa ya gesi bado tumeendelea kupambana kupata nishati ya mafuta ya kuendeshea vyombo vya usafiri na viwandani , nishati ambayo imeendelea kupanda bei kila kukicha.

Sasa hivi inaelezwa, kampuni kubwa za kuunda magari duniani zinatengeneza aina ya magari yasiyotumia kabisa mafuta na yapo baadhi ya mataifa yameshatangaza muda wa mwisho wa kutumika kwa magari yanayotumia mafuta ikiwemo nchi ya Uingereza.

Taifa lina wajibu mkubwa wa kuendeleza uwekezaji mkubwa katika sekta ya nishati hasa kupata vyanzo mbadala kama vile matumizi ya gesi, ambayo yatawezesha kwa kiasi kikubwa kupunguza makali ya maisha si kwa wenye magari tu bali kwa wananchi wote kwa ujumla.

Soko la gesi duniani linazidi kutanuka, hasa kutokana na ukweli kuwa ni nishati rafiki kwa mazingira na sasa nchi nyingi duniani zinapambana kulinda mazingira ambayo yanaharibiwa kila kukicha na vyanzo mbalimbali ikiwamo viwanda, ukataji miti na hata moshi wa magari katika harakati mbalimbali za maisha ya mwanadamu.

Niendelee kutetea kuwa mwanzo mzuri, kinachopaswa kuendelezwa ni maboresho kuwa na Tanzania yenye maendeleo.

# DAWASA kuondoa mabomba chakavu

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imepanga kuondoa miundombinu chakavu ya majisafi katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Miundombinu hiyo yenye umbali wa kilomita 400, itaondolewa katika mwaka huu wa fedha (2023/24) ili kuimarisha huduma na kudhibiti maji yanayopotea kutoka asilimia 37 hadi asilimia 20.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Kiula Kingu alipozungumza na waandishi wa habari jijini.

"Miundombinu ya maji katika Jiji la Dar es Salaam ni ya muda mrefu, kuanzia mwaka 1970 na kuendelea. Mabomba mengi ni ya chuma na yameshapoteza uwezo wa kuhimili kiwango cha maji kinachozalishwa sasa tofauti na miaka ya nyuma, hivyo kusababisha uvujaji mkubwa wa maji katika maeneo mengi tunayohudumia," alisema.

Kingu alitoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa DAWASA kwa kutoa taarifa bila kuchoka wakati mamlaka inaendelea na jitihada za kubadilisha mtandao ya majisafi ambao kwa sasa ni zaidi ya kilomita 7,000.

"Tumeweka nguvu kubwa katika mapinduzi ya teknolojia ili kugundua upotevu unapotokea kwa utaalamu wa kisayansi zaidi huku tukiendelea kutumia mafundi kwa haraka zaidi na kufanyia kazi," alisema Kingu.

Hivi karibuni Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, aliitaka DAWASA kwenda na kasi ya mabadiliko ya teknolojia kwa kuanza kutumia mita za malipo ya kabla ya matumizi ya maji.

Akizungumza wakati wa hafla ya kutia saini makubaliano ya utekelezaji miradi ya maji baina ya DAWASA na Kampuni ya Shanxi, wilayani Kibaha, Mkoa wa Pwani, Waziri Aweso alisema kuna umuhimu wa kwenda na kasi ya dunia ya kidijitali.

Waziri Aweso alisema mita za kulipa kabla ya matumizi zitasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa malalamiko ya wananchi kuhusu bili za maji kwa wengine kudai kupewa bili kubwa kuliko matumizi yao.

Alisema wataalamu wa Wizara ya Maji wanapaswa kuweka mikakati ya kuhakikisha wanaondokana na utaratibu wa sasa wa kulipa bili baada ya matumizi ya maji.

"Huu ni wakati sahihi kwa DAWASA na mamlaka zingine kuanza kutumia teknolojia hii ya mita za kulipa kabla kwasababu zitasaidia kuleta mageuzi nchini kwenye utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi," alisema Aweso.




Rais Samia Suluhu Hassan akimkabidhi tuzo ya Rais ya uzalishaji bora ya mwaka 2023 Mkurugenzi Mkuu wa kiwanda cha NIDA Textile Mills Ltd, Hamza Rafiq ,tuzo hizo za 17 ziliandaliwa na Shirikisho la Wenye Viwanda nchini (CTI), NIDA textile mills Ltd walipewa tuzo hiyo ya uzalishaji bora katika bidhaa za vitenge, khanga na mashuka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Magonjwa ya macho yatikisa halmashauri

**Na Mwandishi Wetu,**
MKURANGA

MAGONJWA tishio ya macho yanayosababisha upofu, hasa trakoma, mtoto wa jicho (cataract) na presha ya macho, yanatajwa kutishia ustawi wa wakazi wa Mkoa wa Pwani baada ya utafiti kubaini kuwapo tishio hilo katika halmashauri saba kati ya tisa.

Akizungumza jana katika Wilaya ya Mkuranga, Mratibu wa Shughuli za Macho wa Mkoa huo, Dk. Eligreta Mnzava, alisema tatizo ambalo ni kubwa zaidi na linasababisha upofu usiozuilika ni la mtoto wa jicho.

Kampeni ya upimaji macho katika Wilaya ya Mkuranga inafadhiliwa na Taasisi ya Al Atar A' Charitable Foundation (ACF).

"Ukiangalia katika wagonjwa tunaowaona kila siku, wengi ni wale wenye mtoto wa jicho. Watu wengi sana wanaopata ni watu wenye umri mkubwa. Huwa wanapata giza kwenye kioo cha jicho. Kwahiyo, tunawagundua na kuwasaidia kufanyiwa operesheni na kufanya waone kabisa.

"Kwahiyo, ninatoa rai kwamba siyo watu waje tu Mkuranga, si kama Mkuranga tu ndiyo wenye tatizo, Mkoa mzima tuna halmashauri tisa na zote kwa kweli zina shida karibia zinafanana.

"Lakini tatizo lingine ambalo linakuja kwa kasi, ni tatizo la presha ya macho. Hili ni tatizo pia ambalo linaleta upofu. Mtu anayeumwa huwa hajui, kwa sababu haliumi, lakini linapoteza uoni.

"Mtu akishafikisha miaka 40 na kuendelea aje kwenye kliniki za macho, apime presha yake ya macho ajulikane ikoje, sababu anaweza kujishtukia anapoteza uoni," alisema.

Ofisa Uhusiano na Mratibu wa Kambi za Macho wa Taasisi ya Al Atar A' Charitable Foundation, Abukari Mbegu, alisema lengo kubwa ni kuwafikia watu 500 na kuwafanyia operesheni ya macho watu 50 na kuwapa miwani ya kusomea watu 150.

Mbegu alifafanua, "katika hizi kambi za afya, tunadhaminiwa na Taasisi ya Kimataifa ya Quatar Charity. Leo (jana) tupo hapa Mkuranga kwa ajili ya kufanya kambi ya macho kwa muda wa siku mbili na vyote hivyo tutavitoa bila gharama yoyote.

"Tumeshafanya kambi kama hii Ngerengere (Morogoro), Sikonge na Kitunda (Tabora), maeneo haya yote malengo yetu ni hayohayo na tumekuwa tukijitahidi kuyafikia. Tukitoka hapa tunakwenda Bagamoyo."

Mmoja wa wanufaika wa kambi hiyo, Rehema Alli, alisema kwa muda mrefu amekuwa anasumbuliwa na macho kuuma na kuwa mekundu, wamenichunguza, wamegundua tatizo lake na wamempa dawa.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# 500 kupata ajira za uuguzi nje ya nchi

**Na Mwandishi Wetu**

NCHI ya Saudi Arabia imekubali kutoa ajira 500 kwa wauguzi wa kike baada ya kuingia makubaliano ya ushirikiano katika masuala ya kazi na Tanzania.

Hayo yalibainishwa juzi mkoani Dar es Salaam na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Cyprian Luhemeja, alipokuwa anatangaza fursa baada ya kutiwa saini kwa hati hizo.

Alisema hati hizo zilizotiwa saini, zinatoa fursa za ajira kwenye mataifa husika kwa kada na sekta zenye kutumia ujuzi wa chini, kati na juu.

"Rais ameelekeza mazungumzo yanayoendelea kwa ajili ya uingiwaji wa mikataba katika nchi 10 yakamilike kwa haraka, ili kuwapatia watanzania wengi fursa ya ajira nje ya nchi. Lengo mazungumzo haya yakamilike Januari 2024," alibainisha.

Alisema watanzania wote wenye sifa na ujuzi uliobainishwa wanatakiwa kuomba kazi husika kwa kujisajili na kutuma wasifu binafsi kwa njia ya barua pepe mwisho wa kutuma maombi hayo ni Desemba 31, mwaka huu na yanapaswa kamilka kabla ya Januari 10, mwakani.

"Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Prof. Joyce Ndalichako, ameelekeza kukutana na watanzania watakaokuwa wamefanikiwa katika mchakato huu Januari 10, mwakani. Waliojiandikisha tayari wawasilishe wasifu (CV) kwa njia ya barua pepe esu@taesa.go.tz," alisema.

Kumekuwa na changamoto ya fursa ya ajira kwa vijana nchini, changamoto ikikua zaidi kuanzia mwaka 2015 serikali ya awamu ya tano ilipoingia madarakani na kusisitisha ajira serikalini kwa takriban miaka mitatu.

Serikali ilisitisha kutoa ajira mpya ili kufanya uhakiki wa watumishi kwa lengo la kuwaondoa katika oorodha ya utumishi wa umma, watumishi 'hewa', waliokuwa na vyeti vya kugushi na watumishi wawili au zaidi waliotumia cheti kimoja kupata ajira serikalini.

# Wafanyakazi NMB watoa mil. 11/- kusaidia matibabu ya watoto JKCI

**Na Mwandishi Wetu**




Kaimu Mkuu wa Idara ya Wateja Binafsi wa Benki ya NMB, Ally Ngingite (kulia), akikabidhi sehemu ya msaada wa vifaa tiba kwa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe, Dk. Yona Kabata (kushoto) vilivyotokana na michango ya wafanyakazi wa Idara ya Wateja Wadogo na Biashara wa benki hiyo. Wa pili kushoto ni Muuguzi wa hospitali hiyo, Flora Mchaina, Meneja Mikopo ya Nyumba Benki ya NMB, Miranda Lutege (wa pili kulia) na Meneja Mahusiano Mwandamizi NMB, Pendo Massawe (katikati). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

WAFANYAKAZI wa Idara ya Wateja Wadogo na Biashara ya Benki ya NMB, wameikabidhi Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) Sh. milioni 11.5 kusaidia kulipia gharama za matibabu ya watoto wenye uhitaji inaowatibu.

Pia wametoa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 1.7 kwa Wodi ya Watoto ya Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe, mkoani Pwani.

Kwa nyakati tofauti juzi, Kaimu Mkuu wa Idara ya Wateja Binafsi wa NMB, Ally Ngingite, alikabidhi kwa niaba ya wafanyakazi hao hundi ya mfano ya kiasi hicho kwa Mkurugenzi wa Huduma za Uuguzi JKCI, Dk. Robert Aloyce na vifaa tiba kwa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe, Dk. Yonna Kabata.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo jijini Dar es Salaam, Ngingite alibainisha kuwa kiasi walichotoa, kimetokana na michango ya wafanyakazi wa idara hiyo na nyongeza kutoka benki yake.

Alisema kuwa lengo lao ni kugusa maisha ya wenye uhitaji katika jamii. Hufanya hivyo kila mwishoni mwa mwaka kupitia idara mbalimbali na ofisi za matawi yao kote nchini.

"Tunaamini kwa kiasi hiki tunachokabidhi, tutakuwa tumeyagusa na kuokoa maisha ya watoto walio katika 'hatua mbalimbali za matibabu hapa JKCI, ili waweze kufanyiwa upasuaji na baada ya hapo tunawaombea uponaji wa haraka kuwawezesha kuendelea na maisha yao ya kawaida. "Hii yote ni kusapoti uwekezaji mkubwa ulilofanywa na serikali katika sekta ya afya, tumepita idara mbalimbali kujionea hilo na sisi kama wadau tukajiona tunao wajibu na uwezo wa kuunga mkono hilo.

"Tumekuwa tunafanya hivi kila mwishoni mwa mwaka kwa wafanyakazi wa benki yetu kupitia idara na ofisi za matawi kote nchini kujichanga mishahara yao na kuangalia maeneo ya kusaidia iwe kwa yatima ama wagonjwa kama hivi," alibainisha Ngingite.

Mkurugenzi wa Tiba Shirikishi wa JKCI, Dk. Delila Kimambo, alishukuru NMB kwa msaada waliotoa kwa watoto hao wanaotibiwa na taasisi yake na kwamba kiasi hicho kinakwenda kugusa pakubwa mioyo na maisha ya wanufaika miongoni mwa watoto wanaotibiwa huko.

"Mlichofanya hapa ni jambo kubwa, mmewapa watoto hawa na wazazi ama walezi wao, mwisho mzuri wa mwaka, tayari kwa kuingia mwaka mpya na matumaini mapya.

"Kwa niaba ya watoto hawa, sisi JKCI tunawashukuru wafanyakazi wote na NMB kwa ujumla kwa kuisapoti serikali ambayo imefanya uwekezaji mkubwa sana hapa unaopaswa kuungwa mkono na wadau wa afya kama hivi mlivyofanya ninyi," alisema Dk. Delila. Kwa niaba ya watoto wengine, Pili Khalfan wa Maneromango mkoani Pwani, ambaye ni mama mzazi wa mmoja wa watoto walionufaika, alisema msaada huo umekuja kwa wakati kwa kuwa alielemewa na gharama za matibabu kiasi cha kukata tamaa, hasa baada ya kutengwa na ndugu pamoja na kukimbiwa na baba wa mtoto wake.

"Nimekuwa napata wakati mgumu, kulala kwangu shida, kula yangu na mtoto ni shida. Aliwahi kutokea mfadhili wa kusaidia matibabu ya mtoto, lakini bima aliyokatiwa tukaambiwa ni ndogo, hivyo haitoshi kugharamia upasuaji wa moyo.

"Leo (juzi) NMB inakwenda kunifuta machozi mimi na mwanangu kusaidia gharama za matibabu yake. Ninaitakia mafanikio yaliyotukuka benki hii, ili iweze kuendelea kusaidia wenye uhitaji wengi zaidi," alisema Pili wakati akitoa neno la shukrani kwa niaba ya wazazi na walezi wenzake.

Kutoka Kisarawe, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya hiyo, Dk. Kabata, hakusita kuipongeza NMB kwa msaada wa vifaa tiba, ambavyo si tu vitawasaidia watoto hospitalini huko, bali pia vinawapa wepesi katika kutoa huduma kwa makundi ya watoto wanaotakiwa kufanyiwa upasuaji na wale wanaohitaji matibabu ya kawaida.

"Kwa niaba ya uongozi wa Hospitali na wagonjwa wote, nitumie nafasi hii kuwashukuru sana NMB kwa msaada huu wa vifaa tiba, ambavyo mnaweza kuona ni mdogo, ila niwahakikishie ni mkubwa na huenda ingetuchukua muda mrefu kuvipata.

"Hapa zipo baadhi ya huduma za bure kwa watoto, lakini wahitaji ni wengi, hivyo huongeza changamoto ya kuishiwa vifaa na mwingine kuvikosa. Hii isiwe mara ya mwisho, mtukimbilie kila mtapokuwa na fungu la kusaidia, itaokoa maisha ya wagonjwa wetu," alisema Dk. Kabata, mbele ya Muuguzi Mfawidhi, Sista Barikian Ngona na Muuguzi wa Wodi ya Watoto, Flora Mchaina.

## 'Mashirika dini yasitumie vibaya misamaha ya kodi'

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MWENYEKITI wa Bodi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania, Mwantumu Mahiza, ameyataka mashirika hayo, yakiwamo ya madhehebu ya dini, kuacha kutumia vibaya hati za hisani zinazotolewa na serikali kwa ajili ya misamaha ya kodi.

Alitoa angalizo hilo mjini Morogoro wakati wa mkutano mkuu wa mwaka wa Chama cha Uzazi na Malezi Bora Tanzania (UMATI) jana.

Alisema yapo baadhi ya mashirika yasiyo ya kiserikali, yakiwamo ya dini, yanatumia vibaya misamaha ya kodi tofauti na malengo ya serikali na kuyataka kuacha kufanya hivyo.

Mwenyekiti huyo alishauri asasi zinazokidhi vigezo kwa ajili ya kupata hati za hisani (misamaha ya kodi) kuwasilisha maombi yao katika Mamlaka ya Mapato (TRA) ambayo tayari dirisha dogo limefunguliwa kuanzia Desemba mwaka huu na kuendelea hadi Februari mwakani.

Alitoa kauli hiyo kufuatia hoja iliyowasilishwa na UMATI kwenye mkutano mkuu wa mwaka kwamba imeshindwa kupata hati ya hisani, tangu ilipoanza kazi zake nchini miaka 62 iliyopita licha ya shughuli wanazozifanya kutokuwa za kibiashara.

"Tunayashauri mashirika haya pamoja na UMATI wapeleke maombi yao TRA kupitia dirisha dogo ambalo tayari limefunguliwa kuanzia Desemba 2023 na kuendelea hadi Februari 2024," alisema.

Mwantumu alisema baadhi ya mashirika ya siyo ya kiserikali yanatumika vibaya misamaha hiyo, hivyo kusababisha hasara kwa serikali.

"Si kwamba misamaha haitolewi, hiyo haki inatolewa, lakini mlolongo wake ni mkubwa imeletwa mahususi," alisema.

Aliongeza kuwa jambo hilo amelizungumza na kujadiliwa na pande zote, lakini shida kubwa watu hawasemi ukweli, hata mashirika ya madhehebu ya kidini au ya kiimani yanaingia katika mkumbo huo wa kutokuwa na uaminifu.

"Utakuta shirika linaomba msamaha wa kodi kuhusu kusamehewa makontena ya vifaa vya kusaidia watoto yatima na wasiojiweza. Serikali inatoa msamaha wa mamilioni, ukaguzi ukienda kufanyika utakuta ndani yake kuna vifaa ambavyo havikupaswa kusamehewa kodi," alisema.

Mwantumu pia alipongeza UMATI kwa kufanya vikao na kuwasilisha taarifa kila robo mwaka kwa msajili na kufanya mkutano mkuu wa kila mwaka kwa mujibu wa sheria inavyowakata na kuitaka iwajengee uwezo wa kiuchumi vijana ili waendelee kujitegemea.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa UMATI, Suzana Mkanzabi, akiwasilisha salamu za chama hicho mbele ya Mwenyekiti huyo wa Bodi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania, alisema chama hicho madhumuni yake makubwa ni kuhakikisha watanzania wanapata afya bora na wanapanga uzazi kwa ajili ya taifa la kesho na la baadaye.

"Ninaomba niwekwe msisitizo mbele yako mgeni rasmi ya kwamba mara nyingi UMATI wanaposema wanafanya kazi kwenye afya ya uzazi, basi watu wanafikiri kuwa ni wafunga kizazi, jambo hili si la kweli," alisema.

Mkanzabi alisema UMATI ni taasisi isiyo ya kiserikali ambayo inajihusisha na masuala ya afya ya uzazi kwa watu wote, hasa kwa vijana na wanawake. Ni taasisi kongwe inayofanya kazi nchini kwa kushirikiana kwa karibu na serikali kwa zaidi ya miaka 62.



## HABARI KASKAZINI

# Silinde aagiza soko la kahawa kutinga EAC

**Na Mary Mosha,** MOSHI

NAIBU Waziri wa Kilimo, David Silinde, ameielekeza Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB), kuanza kutafuta masoko mapya ya zao hilo katika nchi mpya wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ambazo ni Somalia na Sudani Kusini.

Amesema masoko mapya katika mataifa hayo, yataisaidia TCB kufikia malengo yao ya kutoka kwenye uzalishaji wa tani 82,000 mwaka 2022/23 hadi kufikia tani zaidi ya 300,000 ifikapo mwaka 2025.

Silinde alitoa maelekezo hayo jana katika mji wa Moshi, baada ya kuitembelea bodi hiyo na kujionea shughuli mbalimbali na kupata taarifa ya mkakati wa kuendeleza zao hilo.

Aidha, kwa mujibu wa TCB, kiwango cha unywaji wa kahawa nchini, kimeongezeka kutoka asilimia tano hadi kufikia asilimia saba, huku serikali ikiweka wazi mkakati wake wa kupandisha zaidi kiwango hicho mpaka asilimia 15, ifikapo mwaka 2025/26.



Aidha, Naibu Waziri huyo, ametaka kila mmoja kwenye nafasi yake kuhakikisha anaweka alama ya namna bora ya utendaji kazi wake, hasa kwa mkulima anataka kuona kunapatikana matokeo chanya na yenye tija katika kuongeza mapato.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa TCB, Primus Kimaryo, alimweleza Silinde kwamba bodi hiyo inalenga kuwa kinara wa usimamizi na utoaji wa huduma Afrika, kwa kupanua wigo wa soko la ndani.

Kwa mujibu wa Kimariyo, TCB imepanga kuongeza uzalishaji kwa kufungua migahawa ya kisasa, kununua magari ya kisasa ya uuzaji wa kahawa na kuendelea kutoa elimu ya namna bora ya kutumia kahawa.

Pia alisema kuna mkakati wa pamoja na kuleta wataalamu wa afya, kwa ajili ya kuelimisha jamii na wakulima kuhusu kuondoa dhana potofu ya unywaji wa kahawa.

Alisema kwa sasa kahawa inalimwa katika mikoa 17 hapa nchini, ikiongozwa na Kagera ambayo inazalisha kati ya asilimia 40-50 ya kahawa yote nchini.

# Jinamizi ukatili kingono lazidi kutikisa

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

MATUKIO ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto katika mkoa wa Tanga, yameendelea kuongezeka na kufika 134 hali inayoelezwa kutishia ustawi wao.

Kwa mwaka huu peke yake, watoto 416 wamefanyiwa ukatili wa aina mbalimbali, ukiwamo wa kimwili (112), ukatili wa kihisia (65) na utelekezaji wa watoto (105).

Akizungumzia hali ya ukatili katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya mkoa huo, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Tanga (RMO), Dk. Jasphet Simeo, alisema kutokana na mwenendo huo, iko haja ya mashirika ya kiraia, taasisi za umma na wanaharakati kuongeza kasi ya utoaji elimu.

Alisema pia yako mashauri 956 yaliyoripotiwa katika ofisi za ustawi wa jamii mkoani humo, huku migogoro ya ndoa ikiripotiwa 85.

"Huduma kwa waathirika inaendelea kutolewa kupitia vituo vya afya, Polisi, Mahakama na wadau mbalimbali na elimu dhidi ya ukatili inaendelea kutolewa kupitia mikutano ya vijiji, shuleni na vipindi vya radio,"alisema Simeo.

Katika kikao hicho, Shehe wa Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Tanga, Juma Luwuchu, alisema ukatili wa kijinsia, umekuwa ukileta dosari kubwa kwa mkoa huo.

Kutokana na taarifa hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba aliwaagiza wakuu wa wilaya kuwakamata, kuwaweka ndani na kuwafikisha mahakamani wanaoendesha vitendo hivyo.

"Lazima tuwalinde watoto wetu, haiwezekani baba anamtelekeza mtoto wake, tumfuate huko aliko kisha atuambie ana lengo gani, kumtendea ukatili mwanaye,"alisema Kindamba.



Wakulima na wadau mbalimbali kutoka mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara wanaojihusisha na kilimobiashara wanaofadhiliwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini kwa kushirikiana na shirika la Norgwegian Church Aid Tanzania (NCA-Tanzania) wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kumaliza Kongamano maalum la uchumi kupitia kilimobiashara mjini Moshi hivi karibuni.**PICHA: JAMES LANKA**

# Vinasaba mboga njiani kuzinduliwa

**Na Renatha Msungu,** ARUSHA

KITUO cha Dunia cha Mboga (WVC), kimepanga kuzindua benki kuu ya vinasaba ya dunia ya sekta ya mboga na mazao yatokanayo na viungo, mwezi Machi mwaka ujao.

Benki hiyo, pamoja na mambo mengine, itafanya kazi ya kubaini matatizo mbalimbali yanayoikabili sekta hiyo, ikiwemo shughuli za uhifadhi.

Mkurugenzi Mkuu Mshiriki (Afrika) na Mkurugenzi wa Kanda (ESA) na WVC, Dk. Gabriel Rugalema, alisema benki hiyo itakuwa imesheheni vifaa vya kisasa ambavyo vitasaidia kubaini matatizo mbalimbali ya mazao hayo.

Alisema mradi huo unaotarajiwa kukamilika Disemba mwaka huu, unalenga kuhakikisha usalama na uhifadhi wa muda mrefu wa mbegu za mboga, kwa miaka 99.

"Benki tunayoijenga ina vifaa vingi muhimu, ikiwa ni pamoja na sehemu maalum za kupokea na kusindika mbegu. Mahali pa kukaushia mbegu, pamoja na maabara ya mbegu iliyotengenezwa kwa ufundi cherehani," Dk. Rugalema.

Dk. Rugalema, alisema kituo hicho pia kitajumuisha sehemu maalum ya kushughulikia afya ya mbegu ili kuzalisha zenye kiwango cha juu na kutoa mazao mengi.

WVC ilipata ufadhili wa Dola za Marekani, milioni 6.3 kwa ajili ya uendelezaji wa kituo hicho. Inatekeleza miradi inayofanana na ile iliyoko katika nchi nne za Eswatini, Benin na Madagascar. Benki hiyo ya Vinasaba (Gene Bank), inadumisha mkusanyiko mkubwa zaidi wa vijidudu vya mboga ulimwenguni na viambatisho 65,152 vinavyojumuisha vijidudu vya genera 133 na spishi 330 kutoka nchi 155.

Mbali na vijidudu na viambataisho hivyo, itahifadhi pia nyongeza ya mboga za asili 12,000.



# Walimu 'wamsafishia njia' Samia urais mwaka 2025

**Na Vitus Audax,** MWANZA

UMOJA wa Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania (TAHOSSA) umemchangia na kumtunuku Rais Dk. Samia Suluhu Hassan zaidi ya Shilingi milioni tatu kwa ajili ya kuchukua fomu za kutetea kiti hicho katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika nchini mwaka 2025.

Fedha hizo zimechangwa na wakuu wa shule hizo zaidi ya 3,000 kupitia 'kapu la Mama' kufuatia mkutano wao mkuu wa 18 wa mwaka uliomalizika juzi jijini Mwanza ukihutubiwa na Rais Samia kwa njia ya simu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana juu ya mafanikio ya Mkutano huo, Mhazini wa TAHOSSA, Zamoyoni Uzale, alisema walichanga kiasi hicho cha fedha kwa lengo kumuwezesha samia kuchukua fomu baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutangaza mchakato wa kuanza uchaguzi huo.

"Pamoja na mambo mengine yaliyofanyika katika mkutano huu, jambo kubwa lilikuwa n Kapu la Mama ambalo wazo lake tulilipata miezi minne kabla likiungwa mkono na viongozi na wanachama wote kutokana na kazi aliyoifanya kwa kipindi alichoongoza," alisema Uzale

Uzale, alisema kama walimu wamenufaika sehemu kubwa kutokana na maamuzi yaliyofanywa na Rais Samia katika sekta ya elimu na kutumia fedha za UVIKO-19 kujenga madarasa na kuweka madawati hali iliyopunguza uchangishaji wazazi na wananchi.

" Wakuu wote wa shule na walimu tumepewa vishikwambi kufundishia na kutunza kumbukumbu kisasa, hivyo tukasema lazima tumuunge mkono kwa kukubali kwa kauli moja kumchangia ili aendelee kuongoza nchi yetu," alisema.

Alisema 2025 kama wakuu wa shule za sekondari wataomba kumjazia fomu Rais Samia kupitia fedha walizozichanga ili aendelee kuisimamia nchi na kuhakikisha anatimiza malengo yake kwa kipindi kingine cha kuanzia mwaka huo hadi 2030 na kukiomba Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutengeneza fomu moja ili asiwe na mpinzani ndani ya chama hicho.

Akizungumza kwa njia ya simu katika kilele cha mkutano huo, Dk. Samia aliahidi kuendelea kushirikiana na walimu na kuwasaidia katika utekelezaji wa majukumu yao.

"Tunaendelea kujipanga vyema ili kutimiza matakwa ya walimu, najua kinachowasumbua kwa sasa ni makazi (nyumba) hivyo mwakani tunajielekeza zaidi kujenga nyumba za walimu mbali na miundombinu ya shule tutakayoijenga," alisema.

Alisisitiza kuwa Serikali inaendelea kufanyia kazi maslahi ya walimu ili waweze kufanya kazi kwa moyo ya kuwaandaa wanafunzi kuwa viongozi wa baadaye wa Taifa.



Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi akionyesha Simu 61 ambazo wamezikamata kutoka kwa Wanawake watatu ambao ni Raia wa Burundi walioingia nchini kinyume na utaratibu na kufanya shughuli za wizi wa simu kwenye minada ya Mwanza na Shinyanga, pamoja na wanaume ambao hulala nao kufanya biashara ya ngono na simu hizo wakisha ziiba huzipeleka kwao Burundi kwa ajili ya kuziuza. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Kata yaongezewa sekondari mpya

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KATA ya Bulyanhulu inayoongoza kwa kuwa na shule nyingi katika Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama za sekondari nne na msingi 10, imeongezewa sekondari mpya katika Kijiji cha Kakola ili kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani.

Kata hiyo yenye vijiji sita inatajwa kuwa na idadi kubwa ya watu ambao ni zaidi ya 58,000 ikilinganishwa na kata nyingine hali inayosababishwa na mwingiliano mkubwa wa watu kutokana na kuzungukwa na migodi ya madini midogo na mikubwa.

Hali hiyo inaelezwa kusababisha msongamano wa wanafunzi katika madarasa hususani katika Shule ya Sekondari ya Bulyanhuru yenye wanafunzi 2,007 hivyo kulazimu kujengwa shule nyingine kwa gharama ya zaidi ya Shilingi milioni 603.

Mkuu wa Divisheni ya Elimu Sekondari wa Halmashauri hiyo, Mwalimu Seleka Ntobi, akitoa taarifa ya ujenzi wa sekondari iliyopewa jina la Kakola, alisema ikikamilika itapokea wanafunzi wa kidato cha kwanza kwa mwaka wa masomo 2024 kwani tayari imepata usajili.

Alisema kiasi hicho cha fedha kilitolewa kwa ajili ya kuanzisha ujenzi wa sekondari hiyo mpya na Shilingi milioni 449.932 zimetumika kukamilisha ujenzi na miuondombinu yote.

Sekela, alisema shule hiyo ina vyumba vya madarasa nane, jengo la utawala, Teknolojia na Habari na Mawasiliano (TEHAMA), maktaba, matundu 10 ya vyoo vya wanafunzi wa kike na kiume, vyumba vitatu vya maabara kwa ajili ya masomo ya sayansi na wanafunzi 247 watahamishiwa shuleni hapo kutoa Shule ya Sekondari ya Bulyanhulu. Diwani wa Kata ya Bulyanhulu, Shija Luyombya, alisema mwaka jana walipokea wanafunzi wa kuanza kidato cha kwanza 870 na kusababisha msongamano.

uyombya alisema mwaka huu wamepokea wanafunzi 900, na kwamba sekondari hiyo itaondoa msongamano wa wanafunzi Bulyanhulu na utoro, kuacha masomo na ukatili kwa wanafunzi wanaotoka mbali hasa wa kike.

Mkazi wa Kijiji cha Kakola, Emmanule Justin, alisema wametoa maeneo yao kwa ajili ya ujenzi wa sekondari hiyo baada ya kuwa wanapokea ripoti kuwa baadhi ya wanafunzi kukithiri kwa utoro, kuacha shule na kufanyiwa ukatili wa kijinsia.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme akizungumza baada ya kukagua shule hiyo, alimwagiza Katibu Tawala Mkoa, Profesa Siza Tumbi kuhakikisha anapeleka walimu katika sekondari hiyo haraka iwezekanavyo ili wanafunzi wanaotarajia kuanza kidato cha kwanza wasikose masomo.

# Makalla awabana viongozi ujenzi madarasa

**Na Thomas Wandiba,** SAUT

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla amewaagiza viongozi wa wilaya zote mkoani humo kuhakikisha ujenzi ya madarasa, mabweni na matundu ya vyoo unakamilika kabla ya kuanza kwa muhula mpya wa masomo Januari 2024.

Makalla alitoa agizo hilo juzi katika kikao kazi cha wadau wa elimu kilichoketi kuweka mikakati ya kupokea wanafunzi wanaojiunga na shule za awali, msingi na sekondari mkoani humo ikiwa ni pamoja na ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu ya madarasa.

Alisema halmashauri mkoani humo zinapaswa kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya madarasa kama Serikali ilivyoagiza ili kutoa nafasi kwa wanafunzi waliofikia umri wa kujiunga na shule za awali na waliofaulu kwenda sekondari wajiunge mara moja.

"Sitarajii kusikia mtumishi au kiongozi wa Sengerema anakula sikukuu sehemu fulani ndani ya huu muda wakati mpo asilimia 45 tu ya utekelezaji wa agizo la kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya elimu, fanyeni kazi usiku na mchana harakisheni ili mtoke mlipo na ifikapo mwanzo wa muhula muweze kupokea wanafunzi," alisema Makalla.

Ofisa Elimu Mkoa wa Mwanza, Martine Nkwabi, alisema shule za msingi 991 za mkoa huo zilifanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka huu kwa watahiniwa 92, 655

Alisema kati ya hao, watahiniwa 78, 437 sawa na asilimia 84.7 wakiwemo wavulana 36,397 na wasichana 42,040 wamefaulu na kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwakani.

"Matokeo yanaonyesha asilimia ya ufaulu wa Mkoa imepanda kutoka asilimia 82.63 ya mwaka 2022 hadi 84.72 sawa na ongezeko la asilimia 2.09 na ongezeko hilo limetokana na halmashauri zote saba kupandisha ufaulu ikiongozwa na Misungwi iliyopanda kwa asilimia tano japokuwa ni ya mwisho kimkoa kwa ufaulu," alisema.

Alisema pamoja na uwepo wa miundombinu na vifaa bora shuleni, bado watendaji wa kata, vijiji na mitaa wana nafasi ya kuhamasisha wazazi kupeleka watoto shule na kusaidia programu ya chakula shuleni ili kudhibiti utoro,

ama
ALHAMISI DESEMBA 21, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

## KILA MWAKA WAPYA 42,000...
## Kinachojiri; saratani wengi wanadhani ushirikina, matiti kwa kinamama pekee



## MBEGU MPYA, MAVUNO MAPYA...
## Mdau binafsi katika nyayo za serikali kumhamishia mkulima awe mwagiliaji

Ukurasa 14

### UTAWALA AWAMU YA SITA UKIMALIZA MWAKA…

# Mapinduzi rekodi tiba moyo JKCI maradhi 10; ugeni utalii tiba nchi 20

**Na Yasmine Protace**

HADI sasa kuna mikakati mingi ya uwekezaji katika sekta ya afya nchini, kuleta mageuzi kitaifa katika ngazi zote kitaifa; ndani ya zahanati, vituo afya, hospitali za wilaya na mikoa, hali kadhalika kitaifa.

Vyote vinaangukia ndani ya Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), serikali ikiboresha huduma za afya nchini baadhi ya huduma Watanzania wakalazimika kusafiri ughaibuni kuzifuata.

Staili ya uwekezaji huo iko katika sura mbili; kuwajengea uwezo wa kibingwa madaktari waliopo, pia kuongeza miundombinu na vifaa vya utendaji.

Hivi karibuni, serikali kupitia Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKIC), imeanza kutoa upasuaji mdogo wa moyo bila ya kufungua kifua. Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. John Jingu, anasema ni upasuaji unaobadilisha valvu ya mshipa mkubwa wa damu (Aortic Valve) bila ya kufungua kifua (Transcatheter Aortic Valve Implantation procedure - TAVI).

Upasuaji huo kihistoria, anautaja umeshafanyika kwa wagonjwa watatu wenye umri zaidi ya miaka 70 katika kambi maalumu ya matibabu, iliyofanyika siku mbili chini ya wataalamu wa magonjwa ya moyo na mishipa ya damu wa JKCI na wenzao wa Hospitali ya Starcare ya nchini India.

"Uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali katika sekta ya afya, hiyo ikiwa ni pamoja na kujenga majengo ya kisasa, kusomesha wataalamu na kununua vifaa tiba vya kisasa kumewezesha kufanyika kwa upasuaji huo," anasema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Profesa Mohamed Janab, akizungumza wakati wa uzinduzi wa mashine yenye uwezo wa kutibu magonjwa zaidi ya 10, hospitalini hapo, Dar es Salaam. **PICHA: YASMINE PROTACE.**

Dk. Jingu anafafanua, ni zao la umuhimu wa sekta ya afya, huku akiahidi serikali kuendelea kuboresha huduma ya afya ikiwamo wataalamu katika nchi mbalimbali, warejee kutoa matibabu ya kibingwa nchini.

Hivi karibuni, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akafafanua kwamba katika mwaka wa masomo unaoanza sasa, kuna madaktari 600 waliopewa fursa za masomo zaidi kubobea, wakiwa ni asilimia 92 ya waombaji wote.

Katibu Mkuu Dk. Jingu anafafanua, kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Disemba mwaka huu, JKCI imehudumia zaidi ya wagonjwa 3,000 waliofanyiwa upasuaji mkubwa na mdogo wa moyo na kusisitiza, serikali itaendelea kuhakikisha wananchi wanapata huduma za matibabu ya kibingwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) Dk. Peter Kisenge, anaishukuru serikali kwa kuiwezesha taasisi hiyo ikafanya matibabu ya kihistoria, ambayo hayajafikiwa katika nchi za Afrika hakuna hospitali ya serikali, inayotoa huduma hiyo.

"Serikali ya Awamu ya Sita imetuwekea vifaa vingi ambavyo vimewezesha wagonjwa wa namna hii, ambao ni wengi na walikuwa hawajui waende kutibiwa wapi kufanyiwa matibabu.

"Hata wenzetu walifurahia aina ya vifaa tulivyonavyo ambavyo vimewawezesha wataalamu wetu kufanya upasuaji wenyewe kwa asilimia 90," anasema.

**UTALII TIBA**

Aidha, Dk. Kisenge anasema JKCI imeendelea kuwa kituo cha utalii tiba, wagonjwa kutoka nchi 20 za Afrika zinafika kwenye taasisi hiyo kupata matibabu, akiiomba serikali jengo lingine la kuwahamishia wagonjwa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. Jingu anasema kutibu magonjwa zaidi ya 10, umezinduliwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), mtambo unaotumia hewa tiba yenye mgandamizo ya oksijeni.

Ni kifaa kinachotibu magonjwa zaidi ya 10 na kuifanya Tanzania nchi ya kwanza Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, ya pili Kusini mwa Jangwa la Sahara, kutumia mtandao uliogharimu shilingi milioni 250.

**SAUTI KUTOKA MUHIMBILI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili Profesa Mohamed Janabi anasema kupitia matibabu hayo, mgonjwa huingizwa kwenye kifaa maalumu na kupatiwa tiba kupitia hewa tiba ya oksijeni, iliyogandamizwa kwa asilimia 100.

Anataja wagonjwa watakaonufaika, ni wenye vidonda sugu, ambavyo matibabu mengine yameshindikana kama wanaoumwa sukari, waathirika wa moshi wa lioungua na moto, wenye changamoto za kupungukiwa oksijeni mwilini kama waliozama kwenye maji baharini.

Profesa Janabi anataja wagonjwa wengine, ni wenye upungufu mkubwa wa damu na vigumu kuwaongezea, waliopata ajali na wana majeraha sugu kupona, pia wagonjwa wenye maambukizi kwenye mifupa isiyopona.

Anafafanua, wagonjwa wengine ni waliopata mionzi na zikawaathiri, wenye saratani za koo, njia za chakula na wanaougua tezi dume, waliofanyiwa upasuaji na kuwekewa au kupandikiziwa miili.

Wengine ni wenye changamoto za kusikia, wenye tatizo la usaha kwenye ubongo, shida ya oksijeni kwenye mishipa ya damu na watoto wenye usonji (autisim).

Profesa Janabi, pia anaishukuru kampuni ya kitabibu, ambayo kwa kipindi cha miaka miwili, wakatoa mafunzo kuwaidhinishwa madaktari watatu na wauguzi watano kujifunza na kutumia mtambo huo kuhudumia wananchi.

Ni ushirikiano ambao umegusa katika Chuo Kikuu cha cha Dartmouth, Marekani na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS).

AFYA

# Mabinti nchini wanavyokwepeshwa adha za VVU kwa uwezeshaji wa taasisi ya kimataifa

**Na Beatrice Philemon, aliyekuwa Iringa**

UNAPOZUNGUMZIA Mradi wa Kufikia Malengo katika Kudhibiti Maambukizi Mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU) yaani (Mradi wa EpiC), si wananchi wote mkoa wa Iringa na mingine wanaofahamu.

Upo kimataifa wa miaka mitano, unaotekelezwa na Shirika la FHI 360, ukifadhiliwa na Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kukabiliana na UKIMWI (PEPFAR), pia Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID).

Hadi sasa iko katika mikoa 11, ndani ya halmashauri za wilaya 58 za Tanzania, ukilenga makundi yanayohitaji kipaumbele, wakiwamo wasichana wa rika balehe, miaka 15 hadi 25, walio hatarini kupata maambukizi ya VVU.

Mradi umejikita katika kuwafikia na kuendeleza udhibiti wa janga la VVU/UKIMWI nchini, wakitoa msaada wa kitaalamu na huduma za moja kwa moja, kuondoa vikwazo na kuhamasisha usimamizi wa kutegemea miradi ya VVU/UKIMWI kitaifa, kwa kuboresha programu za utambuzi wa maambukizi, kinga, matunzo na tiba.

Hadi sasa kuna wasichana wa rika balehe na kinamama, pia vijana 18,338 mkoa wa Iringa wameshanufaika nao, wakiwezeshwa kuanzisha biashara, baada ya kupata mafunzo, ikiwamo ya ujasiriamali, usimamizi na matumizi ya fedha, kupitia programu inayoitwa: 'Introduce a new program dubbed: 'Determined, Resilient, Empowered AIDS-free, Mentored and Safe' wa kwa kifupi DREAMS.

Edina Mdundwige, msichana wa miaka 23 kutoka kijijini Chaukeleni, Kata ya Ikweha, Halmashauri ya Wilaya Mufindi, kiwa na wenzake walifundishwa kupanga bajeti, kuweka hisa, akiba na kukopa, pia matumizi ya fedha, kuandaa biashara na kutafuta fursa. Mengine anataja ni uzazi wa mpango, kupima afya na uchumi.



Edina Mdundwige, mnufaika wa mradi, akimuonyesha bidhaa anazotengeza Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), Craig Hart (mwenye koti wa kwanza kulia) na Anna Hofmann, Naibu Mkurugenzi anayeshughulikia masuala ya afya USAID, walipotembelea kikundi chao, katika maadhimisho ya miaka 20 ya Mfuko wa PEPFAR nchini Tanzania. **PICHA: BEATRICE PHILEMON.**

**MAFANIKIO YA MAFUNZO**

"Kupitia mafunzo haya, hadi sasa nimefanikiwa kuanzisha mradi wa kusuka vikapu vya aina mbalimbali, mradi wa ufugaji wa nguruwe, maisha yangu yamebadilika sana tofauti na miaka ya nyuma.

"Kwa sababu, hivi sasa nauza bidhaa zangu nikapata pesa, nina uwezo wa kula milo mitatu kwa siku tofauti na miaka ya nyuma,"anaeleza.

Pia, anataja fedha anazopata kutoka uuzaji vikapu. Vilevile kufuga nguruwe, amenunua pampu za kuweka dawa shambani, mbegu za mahindi, mbolea na fedha inayobaki ananunua malighafi ya kusuka vikapu na ufugaji nguruwe.

Kingine anasimulia mtaji wake umeongezeka kutoka shilingi 100,000, hadi 500,000 za biashara ya ufugaji nguruwe na biashara vikapu; vilevile mtaji wa malighafi vikapu umeongezeka kutoka shilingi 70,000, hadi 200,000/-.

Anajisifu ana uwezo wa kupanga bajeti, akinena "Mafunzo yamenitoa mbali sana, hivi sasa nina ujasiri, ninajiamini, naweza kuendesha biashara yangu bila kuwa tegemezi. Nashukuru USAID, PEPFAR na shirika la FHI-360 kuleta mradi huu katika mkoa wetu."

Mama huyo kijana anarejea alikotoka, akitaja alikuwa na uwezo na uelewa wa chini, hakujua uwekaji hisa, kukopa, kuweka akiba, matumizi ya fedha, hata uzazi wa mpango na mengi ya kiuchumi na kimjamii, hata akasema alikula mlo mmoja na jamiio ikamcheka.

Anasema, ndoto yake sasa ni kuwa ama mfanyabiashara mkubwa, au mkulima na mfugaji wa juu, akiinua mtaji mkubwa kwamba utampaisha kibiashara.

Lengo la Edina sasa, ni kupata walau wa shilingi milioni tatu, kwa ajili ya kuendeleza miradi yake ya kilimo na ufugaji.

**MENEJA MRADI**

Mkurugenzi wa Mradi wa Kufikia Malengo katika Kudhibiti Maambukizi Mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU), Bernard Ogwang, anasema mradi umewasaidia wasichana wa rika balehe.

Kuna suala la kinamama vijana wanabadilisha maisha yao, wakianzisha biashara, wanapata mafunzo ya ufundi stadi, wanaongeza kipato, tiba na uelewa wa kupima afya, VVU.

Anataja kuwa ni mradi unaolenga kupatikana huduma kinga, upimaji, tiba na matunzo, hata kufikia kuendeleza udhibiti wa maambukizi na wanaimarisha usimamizi wa fedha za kutekeleza shughuli hizo, asasi za kiraia izkijengfwa uwezo kupata ufadhili wa moja kwa moja na hata waktekelezaji wa miradi.

"Kupitia mradi huu, tunatoa huduma za moja kwa moja na msaada wa kitaalamu kuhusu kujikinga na kutokomeza VVU kwa kuzingatia ongezeko la upatikanaji wa huduma za kinga, matunzo, tiba na fuatiliaji wa wingi wa VVU mwilini," anasema.

Anasema katika kuwakinga mabinti wa rika balehe na kinamama vijana, wanawake na wanaume walio katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya VVU, mradi unawawezesha kupitia kwa kuiwapa mabadiliko ya kitabia, kuimarisha uchumi na kutoa huduma za kitabibu, wakiiihamsiha jamii kupunguza utamaduni hasi zinazowaathiri mabinti.

**MAFANIKIO YA MRADI**

Ogwang ansema, hadi sasa kuna wasichana wa rika balehe na kinamama vijana 220,123 waliofikiwa na kati yao, wasichana wa rika balehe na kuna kianamama vijana 1294 waligunduliwa kuwa na VVU, 1207.

Hatua iliyochukuliwa, asilimia 93 waliunganishwa kwenye vituo vya Huduma ya Tiba na Matunzo (CTC) kufubaza VVU na 5892 walipewa dawa za kupunguza makali ya VVU (PrEP).

Hadi sasa kunatajwa vikundi 126 vimeshasajiliwa mkoani Iringa, viwili kati yao vimeishapata mkopo wa serikali wenye wa shilingi milioni sita, kuendeleza biashara zao.

Vilevile, Ogwanga ansema, kuna vitovu (Hubs) 16 za uwezeshaji mabinti kiuchumi vimeanzishwa, vitovu viwili vipo katika wilaya ya Mufindi.

Hadi sasa jumla ya wasichana wa rika balehe na akina mama vijana 128 wamemaliza mafunzo kupitia hizo hubs.

Anasema kati ya hao; 78 wamepata mafunzo ya ushonaji; 50 mafunzo ya kompyuta; 25 wamepewa elimu ya ufundi wilayani Mufindi na kupewa vifaa na mahitaji ya kuanzia mradi.

Hadi sasa jumla ya wasichana wa rika balehe na akina mama vijana 2247 wameweza kuanzisha biashara zao binafsi za kilimo, mboga mboga na matunda, uokaji wa bidhaa za aina mbalimbali, ufugaji wa mifugo, ufugaji kuku, maduka ya reja reja, ushonaji na usukaji wa bidhaa mbalimbali za vikapu na bidhaa nyingine.

87 wameungwanishwa na bima ya afya ya jamii (CHF), 11 wameunganishwa na kituo cha Elimu na Mafunzo ya Ufundi stadi (VETA)- iringa, kati ya hao, saba wanasoma kozi ya welding, wanne wanasoma kozi ya plumbling kwa ufadhili wa serikali ya Ujerumani kupitia shirika lake la Maendeleo la GIZ nchini.

**OFISA MAENDELEO JAMII**

Ofisa Maendeleo ya Jamii, Manispaa ya Iringa, Mwantumu Dosi, anazishukuru mashirika la USAID Na PEPFAR kuleta Mradi wa EpiC mkoani Iringa, wasichana wa rika balehe na kinamam a wamenufaika kwa kufaya shughuli kuu za kufanya na walipata fursa kufanya ziara katika mikoa ya Mwanza na Mbeya kujifunza.

**OFISA MTENDAJI KATA**

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Sadaani (WEO), Marcus Makweta, anasema ni mradi unaowafanya mabinti wakae sehemu moja kujifunza, wao wakiwa na vyerehani 10 , mabinti wanajifunza.

Wanufaika wa Mradi, wanawaomba wadau na serikali wawasaidie, kupata kituo cha mafunzo ya ufundi katika Manispaa ya Iringa, mabinti wengi wanufaike kama wenzao wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.

AFYA

## KILA MWAKA WAPYA WANAOJITOKEZA 42,000…

# Kinachojiri; saratani wengi wanadhani ushirikina, matiti kwa kinamama pekee

## •Ummy: Rais kaweka mashine kila mkoa, tukapime

**Na Christina Mwakangale**

"NI tatizo la muda mrefu, si unajua familia za kiswahili akaambiwa karogwa na mkewe. Kwa uvimbe wake huo, ilionekana karogwa, mara afanyiwe tambiko, mara wadai mkewe anataka kumfanya msukule."

Hiyo ni kauli ya mmoja wa wanafamilia, mkazi wa Dar es Salaam, ambaye hakuwa tayari kuandika jina lake gazetini. Anaeleza kile kilichotokea kwenye familia yao, baada ya ndugu yao kuugua kwa muda mrefu.

Anasema licha ya kwamba wataalamu wa afya kuthibitisha ndugu yao anaugua saratani ya matiti, mvutano ndani ya familia ulikuwa mkubwa na kusababisha baadhi yao kutoelewana, wakidai matokeo ya maradhi ni kurogwa.

"Chanzo ni uvimbe tu, hamna lingine zaidi ya hilo. Hiyo ya saratani ya matiti kwa wanaume ni kweli, mimi baba yangu mdogo kifo chake kimetokana na tatizo hilo.

"Tatizo familia zetu hizi. Ikavumishwa mke wake ndio kamroga, matokeo yake yule mama mdogo hana hamu na familia, mimi nilikwenda hadi Muhimbili (Hospitali ya Taifa), kwenye vipimo, walimchunguza kwenye titi lenye uvimbe, ikatoka damu nyeusi sana, sitasahau," anasimulia kile anachokielewa.

Wakati hayo yakijiri katika baadhi ya familia nchini kukiwapo jumla ya wazi katika nchi yenye watu milioni 61, kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi na mwaka 2022, inakadiriwa kila mwaka kuna wagonjwa wapya wa saratani 42,000.

Aidha, katika mwezi maalum wa kuhamasisha jamii juu ya uelewa kuhusu saratani ya matiti ambao ni Oktoba ya kila mwaka, umechaguliwa utumike kutoa elimu na kuhamasisha jamii juu ya yaliyo umuhimu kuchunguza mapema njia bora za kuzuia maradhi ya saratani ya matiti.

Hapo kunashuhudiwa asasi na wadau tofauti kama vile ubalozi wa Sweden nchini wakiuadhimisha katika siku maalum.




Mandhari ya Taasisi ya Kansa Ocean Road, Dar es Salaam.

### WADAU WAFUNGUKA

Balozi wa Sweden nchini, Charlotta Ozaki, katika mkutano na waandishi wa habari, Dar es Salaam, anasema asilimia 6.5 ya wagonjwa wote wa saratani nchini wanatajwa ni wanaume, kwamba idadi hiyo ni mara 10 zaidi ya saratani inayoonekana nchi nyingi duniani.

Anasema, pamoja na maadhimisho ya miaka 60 ya ubalozi huo kuwapo nchini, ushiriki wao katika kampeni ya kupambana na saratani ya matiti nchini nao kwa sasa ni mkubwa.

"Tunataka kuongeza ufahamu kuhusu saratani ya matiti kwa wanaume hata wavulana na kuwasaidia wanawake. Tunataka watu wajifunze saratani ya matiti sio ugonjwa wa wanawake tu, wanaume pia huathiriwa," anasema Ozaki.

Balozi huyo ambaye pia ni shujaa wa saratani ya matiti, anasema kwamba nchini saratani ya matiti imeripotiwa kwa kiasi kidogo katika miongo miwili iliyopita, pia kukiwapo utafiti mdogo.

"Iwapo hakutakuwa na juhudi za dhati, ongezeko la visa vipya vya saratani Tanzania, inakadiriwa kufikia asilimia 82 ifikapo mwaka 2030," anaeleza balozi huyo.

Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa SCF, Gloria Kida, anasema, matembezi yatakayofanyika yanalenga kukuza uelewa kuhusu umuhimu wa kupima saratani ya matiti na kujipima, pamoja na kusaidia walioathirika umuhimu wa utafiti, kuzuia, matibabu na kupona.

Kida anasema, sambamba na hayo kutakuwapo matembezi na mafunzo yatakayotolewa, pia kuhusu teknolojia ya kisasa zaidi katika kuchunguza saratani nchini, Sweden ikiwa sehemu ya mfadhili.

### SERIKALI YAFAFANUA

Katika ufafanuzi wake wa mwezi husika wa elimu, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anasema: "Wataalamu wanatueleza kwamba mtu anaweza kujichunguza mwenyewe na akiona mabadiliko ya uvimbe katika titi, basi anashauriwa kuwahi katika kituo cha kutoa huduma za afya kwa uchunguzi zaidi.

"Tanzania inakadiriwa kuwa na wagonjwa wapya wa saratani takribani 42,000 kila mwaka, ambao wanafika katika vituo vya kutolea huduma za afya. Kila mwaka, kati ya hao wagonjwa, asilimia 38 tu ndio wanafika hospitali.

"Maana yake, katika kila wagonjwa 100 wa saratani, wagonjwa 38 tu ndio wanafika katika vituo vya kutolea huduma za afya."

Pia, anasema taarifa ya mwaka 2022/2023, inaonyesha kuwa Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), ilihudumia wagonjwa wapya takriban 8,779 na asilimia 13 ya wagonjwa hao ambao ni 1,141 walikuwa na saratani ya matiti.

Waziri Ummy anamshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuiwezesha wizara hiyo, kufunga mashine za uchunguzi - 'CT-Scan' katika hospitali zote za rufani na mikoa na mashine za 'Ultrasound' katika hospitali zote za halmashauri nchini.

"Hii inamaanisha uchunguzi na ugunduzi wa saratani ya matiti, unaweza kufanyika katika hospitali, ikiwamo za rufani za mikoa na halmashauri," anasema Ummy.

Hivyo, Waziri Ummy anatoa wito kwa wananchi kuhakikisha wanafanya vipimo katika hospitali angalau mara moja kwa mwaka, hasa kwa wanawake na ikigundulika wana tatizo, matibabu yaanze mapema.

"Hata wanaume wanatakiwa kupima kwa kuwa, katika kila wagonjwa wa saratani ya matiti 100, wagonjwa 99 ni wanawake na mmoja ni mwanaume. Tunawaomba wananchi wawahi katika vituo vya kutolea huduma za afya, ili kupima na kupata matibabu mapema," anasema Ummy.



Huduma za tiba ya kansa zikiendelea. **PICHA ZOTE; MTANDAO.**

MAZINGIRA

### MBEGU MPYA, MAVUNO MAPYA KUPAMBANA NA TABIA NCHI…

# Mdau binafsi katika nyayo za serikali kumhamishia mkulima awe mwagiliaji

**Na Maulid Mmbaga, alioyekuwa Dodoma**

BAADA ya kilimo cha kutegemea mvua kuonekana kikwazo hata kusababisha kuchelewa uzalishaji mazao, wadau wa maendeleo wanashauri wakulima kuhamia kwenye umwagiliaji, njia ambayo utekelezaji wake umebainishwa kuongeza tija zaidi ya uzalishaji mbegu ya alizeti.

Kilimo kikiwa mama, kutoa fursa za ajira kwa takribani asilimia 65 ya Watanzania, serikali iliamua kuongeza bajeti yake kutoka Sh. Bilioni 751.12 hadi Sh. Bilioni 970.78 kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuboresha Mifumo ya Masoko ya Kilimo Tanzania (AMDT) Charles Ogutu, akizungumza siku chache zilizopita mkoani Dodoma, kwamba kupitia kilimo cha umwagiliaji, wanaamini mbegu za alizeti na jamii ya mikunde ndani ya miaka mitatu au minne zitapatikana kwa wingi nchini.

Anasema mikakati yao, wanataka mbegu hizo za alizeti zizalishwe nje ya msimu wa mkulima wa kawaida, ili inapofikia msimu husika wa kulima mkulima awe tayari ana mbegu.

"Kazi hiyo tayari tunafanya na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Ilonga, tunawawezesha na kuwafungia mfumo wa 'drip irigation' umwagiliaji, kwa ajili ya kuzalisha mbegu za alizeti na nadhani itakuwa ya kwanza na waziri mwenye dhamana alivyoona alifurahi sana," anasema Ogutu.

Anaendelea: "Tayari mfumo umeshafungwa, japo ulichelewa kidogo kutokana na taratibu za kiserikali na bahati nzuri, tulipata kibali cha Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akasema 'next time' tusifanye hivyo. Tukubaliane nao, sisi tupeleke sekta binafsi wao watupe eneo lifungwe mfumo, ibakie kazi ya kwao ya kuzalisha mbegu."

Ogutu anafafanua kuwa, jamii kubwa ya watu wana chachu ya kuhitaji elimu, uelewa na taarifa sahihi wanazopata, wanaweza wakabadilika kutoka kwenye kilimo cha mazoea.

"Nilipita Mererani ni kukavu, lakini watu wamechimba visima ukiangalia mazao unashangaa alizeti imechanua kwenye mashamba, lakini huku kwengineko kote ni vumbi ni kukavu kabisa kwa hiyo kuna mengi, tunayohitaji kuyafanya, ili kuhakikisha inakuwa na matokeo makubwa," anasema Ogutu.

**KWANINI ALIZETI**

Mkurugenzi huyo anaeleza kuwa wamechagua kutoa kipaumbele kwenye zao la alizeti na jamii ya mikunde, kwa sababu ni mazao ya kimkakati kwenye Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (SDPII).

Anasema katika programu hiyo, alizeti imeainishwa kama 'bidhaa muhimu' inayoweza kulisaidia taifa kupunguza gharama kubwa kuingiza mafuta ya kula kutoka nchi za nje.

Pia, anasema mazao yote wanayoshughulika nayo yako katika mkakati wa serikali na yameonyeshwa umuhimu wake, na kwamba wanachokifanya ni kuona ni namna gani wanaweza kuchangia katika mpango mzima wa taifa.

"Ili wakulima waweze kuhimili mabadiliko ya tabianchi, kunahitajika mbinu na mikakati mbalimbali, lakini mazao haya yana umuhimu wa kipekee, mfano ukichukua jamii ya mikunde ukayachanganya na alizeti na mahindi inawafanya wakulima wamudu ustahimilivu.

"Ustahimilivu huo unakuwa mkubwa, kwa sababu mazao hayo yanavumilia, hayahitaji mvua nyingi. Wanapoyalima, wanavuna na hayakai sana shambani, pia yanasaidia kurutubisha afya ya udongo na mkulima hatahitaji sana mbolea za viwandani," anatamka Ogutu.

Frank Chipanta, kutoka shirika la Adda Tanzania, anasema kwa kushirikiana na AMDT na Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) wametoa elimu ya uzalishaji mbegu za alizeti kwa wakulima, na kwamba kupitia ufadhili wa taasisi kutoka Denmark iliwasaidia kuwawekea miundombinu ya umwagiliaji shambani.

Anasema, msimu uliopita walifanya majaribio ya kilimo cha umwagiliaji kwa zao alizeti, lengo lao ni kuviimarishia vikundi vya wakulima kuzalisha mbegu za alizeti, ili kusaidia wakulima wenzao wadogo.

**MAFANIKIO YA WAKULIMA**

Mwenyekiti wa MVIWATA, Omary Mpapati, anasema baada ya kuvuna, wameona kilimo hicho ni bora zaidi, kwakuwa awali walikuwa wanavuna gunia moja, lakini kwa sasa wanapata zaidi ya gunia tatu kwa ekari.

Mkulima anayejihusisha na kilimo cha umwagiliaji katika kijiji cha Mkoka Wilayani Kongwa, Victoria Mweria, anasema baada ya kupata mafunzo na kuanza utekelezaji, walibaini fursa ya kulima bila kutegemea mvua.

"Tumelima na kwa kiasi kikubwa tumefanikiwa kuvuna alizeti kwa wingi tofauti na kilimo cha kawaida na imebadilisha hata mfumo wa maisha yangu. Nimehamasisha wanawake wenzangu kujiunga na kilimo hiki kwa sababu kinatutoa na kutufikisha mbali kimaisha.

"Ninaona mabadiliko, kwasababu, kwanza nimepata elimu na nimeweza kuwarithisha wengine, mwanzo tulikuwa tunalima kiholela, lakini sasa hivi tunafanya kitaalamu.

"Pia, nitakuwa mwalimu wa wanawake wenzangu ambao hawajaelewa faida ya kilimo hichi cha umwagiliaji," anasema Victoria.

Katibu wa Kikundi cha Wakulima cha Mkoka, Oziniel Benego, anasema wamepata faida kubwa kutoka AMDT, baada ya kufanikiwa kupata wataalamu 20 waliosomeshwa juu ya kufanya kilimo hai na namna ya uzalishaji wa mbegu za alizeti.

Hata hivyo, anaeleza kuwa kwa sasa asilimia kubwa ya wakulima wameshafundishwa namna ya matumizi ya ardhi, mbolea na wamehamia kwenye kufanya kilimo chenye tija, akieleza mabadiliko ya mkulima mdogo yameanza kuonekana.

**CHANGAMOTO**

Benego anaeleza katika kijiji hicho, wakulima wadogo walikuwa wanakabiliwa na changamoto ya kucheleweshwa mbegu zilizokuwa zinawafikia nje ya wakati, na baada ya uzalishaji kuongezeka, kwa sasa wanazipata kirahisi, kwa bei inayoendana na maisha halisi ya mkulima.

"Faida nyingine, mbegu hii wanainunua wakiwa na uhakika kwa maana kwamba wameiona kwa macho toka ikiwa shambani, na mwamko umeongezeka wengi wameanza kujifunza sio tu kwenye kikundi bali hata nje," anasema Benego.

Mwenyekiti wa Mtandao wa MVIWATA, Mpapati, anataja changamoto nyingine inayowakabili, ni kwamba mfumo wanaoutumia sasa kumwagilia wakitumia mifereji, unawafanya kutumia kiwango kikubwa cha maji.

Anatoa wito kwa serikali na wadau mbalimbali wa maendeleo kuwasaidia kupata mfumo mbadala wa kutumia matone, akitaja ni rafiki kwa kiasi kikubwa kutekelezaji kilimo cha umwagiliaji, hasa kwenye maeneo yenye changamoto ya maji.



Mkulima wa alizeti, kwa mfumo wa umwagiliaji kijijini Mkoka, wilayani Kongwa, Dodoma, Victoria Mweria, akionyesha hatua anazopiga shambani kwa ukubwa.




Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuboresha Mifumo ya Masoko ya Kilimo Tanzania (AMDT) Charles Ogutu, akieleza kilimo cha umwagiliaji kilivyoongeza tija katika uzalishaji. **PICHA ZOTE: MAULID MMBAGA.**





# Bilioni 14.5/- kuboresha elimu, afya Dodoma

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imepokea kiasi cha Sh. bilioni 14.3 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo mbalimbali ikiwemo ya elimu na afya.

Mkuu wa Divisheni ya Mipango na Uratibu wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Francis Kaunda, alibainisha hayo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Jiji katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya ya Dodoma kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa halmashauri.

Kaunda alisema kwa kipindi cha Julai hadi Novemba, 2023, Halmashauri ya Jiji la Dodoma imepokea kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

"Kati ya fedha hizo kiasi cha Sh. bilioni 4. 7 ni kutoka serikali kuu, Sh.bilioni 9.7 ni fedha za mapato ya ndani" alisema Kaunda.

Alisema utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 umeleta mafanikio mbalimbali kama vile halmashauri kujenga na kuanzisha shule mpya mbili za mchepuo wa kiingereza za Msangalalee na Dodoma.

"Halmashauri imekamilisha ujenzi na kusajili shule mpya nne za awali na msingi ambazo ni Jitegemee iliyopo Kata ya Mnadani, Mayeto iliyopo Kata ya Hombolo Makulu, Swaswa iliyopo Kata ya Ipagala na Msalato iliyopo Kata ya Msalato.

Mafanikio mengine ni kuanzisha shule mpya ya sekondari ya Mtemi Chiloloma iliyopo Hombolo Makulu ambayo inatoa huduma na shule mpya ya sekondari iliyopo Mpamaa itaanza kufanya kazi mwezi Januari, 2024," alisema Kaunda.

Mafanikio katika sekta ya Afya, aliyataja kuwa ni ujenzi wa vituo vinne vya Afya, kati ya hivyo, vituo viwili vya Nkuhungu na Chang'ombe vinatumika na Kizota na Zuzu vipo hatua za umaliziaji. Zahanati ya Mpamaa na Zepisa zimekamilika na zinatumika, aliongeza.

Akizungumzia mafanikio sekta ya Elimu, alisema kuwa wilaya imeweza kupandisha ufaulu kutoka asilimia 89.2 mwaka 2022 mpaka asilimia 93.18 mwaka 2023. Halmashauri inaendelea na jitihada za kufikisha asilimia 100 ya ufaulu alisema.

# Mwanasheria Mkuu alia upungufu wa watumishi kuathiri ufanisi kazi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali, Jaji Dk. Eliezer Feleshi, amesema ofisi yake inakabiliwa na upungufu wa watumishi 285 hali inayochangia baadhi ya shughuli kushindwa kutekelezwa kwa ufanisi.

Dk. Feleshi alibainisha hayo jana jijini hapa katika hotuba ya ufunguzi wa kikao cha baraza la wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kinachofanyika kwa siku mbili.

Alisema mahitaji kwa watumishi kwenye ofisi yake ni 477 lakini waliopo hivi sasa ni 192, hivyo kufanya upungufu kuwa ni watumishi 285 katika maeneo mbalimbali.

"Tunaishukuru serikali kwa kutoa kibali cha kuajiri watumishi 50 katika mwaka wa fedha 2022/23. Watumishi 48 walikuwa mawakili na wawili ni wataalamu wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA)," alisema.

Aidha, alisema kero nyingine ni vitendea kazi hasa usafiri kwa mawakili wa mikoa na ofisi ngazi hiyo na wilaya hali inayochangia watumishi kushindwa kutoa huduma kwa ufanisi kwa wananchi wa maeneo hayo.

Dk. Feleshi alisema lengo la kikao hicho cha baraza la wafanyakazi ni kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti.

"Pia kupima mafanikio ya mpango wa bajeti, kujadili hoja mbalimbali zitakazoibuliwa na wajumbe wa baraza hili na kuzitafutia ufumbuzi," alisema. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, akifungua kikao hicho, aliwataka watumishi wa umma kuwa wazalendo hasa katika suala linalohusu nchi yao.

"Niwapongeze kwa kuwa wazalendo licha ya changamoto mnazokabiliwa nazo katika utumishi wenu hivi sasa watumishi wengi wa umma wamekuwa siyo wazalendo.

"Hata kama kuna jambo litatokea linalohusu kuumiza nchi wao wala haiwagusi, uzalendo ni jambo la msingi lazima kila mmoja wetu awe nalo moyoni," alisema Mchengerwa.

Kuhusu changamoto mbalimbali zinazoikabili ofisi hiyo Mchengerwa, alimuelekeza Mwanasheria Mkuu wa serikali kukaa na ofisi yake ili kuandaa mpango kazi ambao utasaidia kupata suluhu ya kero mbalimbali.

"Tukae tuandae mpango mkakati ambao utasaidia kutatua changamoto hizi mlizosema kwani TAMISEMI ni ya wananchi, hivyo lazima tuweke mazingira mazuri kwa wananchi kupata huduma hizi kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali"alisema

Hata hivyo, alisema tatizo la ukosefu wa vyombo vya usafiri atalifikisha kwa Rais Samia Suluhu Hassan ili kuona ni jinsi gani italifanyia kazi.

Alisema muhimili wa Mahakama hivi sasa umepiga hatua sana hivyo serikali ina wajibu wa kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazoikabili ofisi hiyo ili kuongeza ufanisi.




Baadhi wananchi wakitafuta mahitaji ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya sikukuu ya Krismas kama walivyokutwa katika eneo la One way lenye maduka mengi Jijini Dodoma jana . **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Tanzania kinara kupunguza vifo uzazi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TANZANIA imekuwa nchi ya kwanza Afrika kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi kwa kinamama kutoka 556 hadi kufikia 104 kwa kila vizazi hai 100,000.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Wilson Mahera, alisema hayo wakati wa hafla ya kukabidhi magari sita yatakayotumika kwa ajili ya usimamizi katika sekta ya afya mkoa wa Singida.

"Tumepunguza sana idadi ya vifo vya akina mama kutokana na juhudi kubwa zilizowekwa katika uwekezaji kwenye sekta ya afya. Tanzania imekuwa nchi ya kwanza kwa Afrika kwa kupunguza vifo kutoka 556 kwa vizazi hai 100,000 mpaka kufikia vifo 104 kwa vizazi hai 100,000," alisema.

Dk. Mahera aliwasihi watumishi wa sekta ya afya kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa huduma zilizo bora na kwamba serikali haitamuonea haya mtumishi ambaye hatataka kutoa huduma bora kwa wananchi.

Alisema kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya watumishi kutoa huduma mbovu kwa wananchi ambao ndio waajiri wa rais na atakayebainika atachukuliwa hatua ikiwamo kusimamishwa kazi.

"Watumishi tuelewane, kikitokea kifo kwa uzembe tutakuchukulia hatua na yeyote atakayekuchukulia hatua na atakayejaribu kumtetea na yeye tutamuondoa kwani wapo Watanzania zaidi ya 100,000 wanaomba ajira," alisema.

Mganga Mkuu wa Mkoa, Victorina Ludovick, utoaji wa huduma za afya umeongezeka mkoani hapa ambapo katika kipindi cha 2022/2023 na 2023/2024 mkoa umepewa Sh.bilioni 7.5 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba.

Alisema kutokana na jitihada hizo za serikali, kumekuwa na ongezeko la upatikanaji wa dawa katika vituo vya afya kwa wastani wa asilimia 95.

Dk. Ludovick alisema katika kipindi cha kuanzia mwaka jana hadi mwaka huu idadi ya vituo vya afya katika mkoa wa Singida vimeongezeka kutoka 259 hadi kufikia 329 na pia huduma za upasuaji zimesogezwa karibu na wananchi kwenye vituo 21 kutokana na kuimarishwa kwa miundombinu.

Aidha, watumishi wameongezeka kufuatia watumishi 329/wa kada mbalimbali kupangiwa kufanya kazi katika Mkoa wa Singida baada ya kuajiriwa katika ajira mpya ambapo kati yao asilimia 96.6 waliweza kuripoti kazini.





# DC akemea uharibifu vyanzo vya maji

Na Elizabeth John, LUDEWA

WANANCHI wilayani Ludewa Mkoa wa Njombe, wameelekezwa kuachana na shughuli za kibinadamu kandokando ya vyanzo vya maji maarufu kama vinyungu ili kutunza mazingira.

Wito huo ulitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Victoria Mwanziva, wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama katika kukagua miradi ya maji ya kata za Mavanga, Ludewa, Iwela na Manda.

Ziara ya mkuu huyo wa wilaya pia imehusisha kutoa elimu kwa wananchi juu ya madhara ya kufanya kilimo jirani na vyanzo vya maji.

Mwanziva alisema miradi ya maji inapaswa kulindwa kwa sababu serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan inaendelea kutoa fedha katika sekta hiyo ili kumtua ndoo mama kichwani.

"Rai yangu kwa wananchi ni kuhakikisha tunatunza vyanzo vya maji na hilo ndilo la msingi, wilaya yetu imebarikiwa tuna vyanzo 150 vya maji, tulitembelea baadhi ya vyanzo na kujihakikishia kwamba wananchi wanaendelea kushirikishwa katika utunzaji wa vyanzo vya maji," alisema Mwanziva.

Aidha, Mwanziva alitoa onyo kwa wakulima na wafugaji kuwa na matukio ya kufanya shughuli za uchungaji wa mifugo na kuendeleza kilimo kwenye maeneo ya vyanzo vya maji waache mara moja kufanya shughuli hizo ili kuweza kuvitunza kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Ludewa, Mhandisi Jeremiah Maduhu, alisema wanaendelea kutoa elimu kwa jamii ili kuhakikisha rasilimali za misitu ambayo ndiyo vyanzo vikuu vya asili vya maji wilayani Ludewa vinalindwa.

"Tunaendeleza Ushirikiano wa idara za mazingira kwa ajili ya mazoezi ya upandaji miti wilayani Ludewa na elimu kwa jamii ili kulinda vyanzo vya maji," alisema.

Maduhu alisema wilaya ya Ludewa inatekeleza miradi saba ya maji yenye thamani ya zaidi Sh. bilioni 13 na itakapomilika itaongeza huduma ya maji kutoka asilimia 74.3 hadi asilimia 79.7 eneo la vijijini na asilimia 100 kwa wakazi wa Mji wa Ludewa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Sanday Deogratius, alisema wamepokea fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji na kuleta mabadiliko makubwa katika sekta pamoja na kutosita kuwachukulia hatua watakaokaidi sheria ndogo za usimamizi wa vyanzo vya maji.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Ludewa Mjini, Wilfred Mwalongo, aliishukuru serikali kwa kuwapelekea mradi mkubwa wa maji utakaowapa ahueni katika changamoto hiyo.

"Ndoa nyingi zilizokuwa zinavunjika kwa kukosekana kwa maji kwa muda mrefu kwenda kutafuta kwenye vyanzo ambavyo sio sahihi, sasa tunaimani tunakwenda kuzihimarisha na kutakuwa hakuna mvunjiko wa ndoa nyingi," alisema Mwalongo.

Mwalongo alisema kama kijiji wamejiwekea mikakati ya kuhakikisha vyanzo vya maji vinatunzwa na kulindwa na visifanyiwe kazi za kibinadamu kwa manufaa ya baadaye.

Awali akisoma taarifa ya mradi wa maji Ludewa mjini, Mkurugenzi Mamlaka ya Maji Ludewa Mjini mhandisi Enock Ngoyinde alisema mradi huo unatekelezwa kwa thamani ya bilioni 7.4 ambapo unahusisha ujenzi wa chanzo cha maji kipya, ujenzi wa matanki mtatu na ujenzi wa laini kuu yenye urefu wa km 21.9.



Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Mkoa wa Njombe, Victoria Mwanziva akipanda juu ya tanki la maji lililopo Ludewa Mjini katika muendelezo wa ziara yake aliyoambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya kukagua miradi ya maji wilayani Ludewa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajawazito walia gharama upasuaji

Na Elizabeth John, MAKAMBAKO

WAJAWAZITO katika Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe, wamelalamikia Kituo cha Afya cha Makambako kwa kitendo chake cha kuwatoza wajawazito fedha sh. 150,000 kwa ajili ya upasuaji.

Malalamiko hayo yalitolewa mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, kwenye mkutano wa hadhara wa kusikiliza kero za wananchi uliofanyika mjini hapa.

Walisema ukifika kituo hicho inapofika muda wa kuchukua dawa unapewa chache na nyingine unaambiwa uende duka lililopo karibu ili kununua hali inayowapa mashaka kuwa dawa walizostahili kupewa bure wanauziwa.

Mmoja wa wananchi hao, Yustina Malekela, alisema kuna wakati wakifika kwenye duka hilo la dawa ili kununua wanakuta dawa ambazo wananunua zimeandikwa kuwa dawa hizo ni za msaada.

Christopher Nason alisema alimpeleka mke wake akiwa mjamzito katika kituo hicho na alipotakiwa kufanyiwa upasuaji aliambiwa alipe kiasi cha sh. 150,000.

"Mimi nilimpeleka mke wangu akafanyiwe upasuaji nikaambiwa bila ya Sh. 150,000 mke wangu hawezi kufanyiwa upasuaji na nililipa na mke wangu akaendelea kufanyiwa upasuaji.

Kilichoniumiza kuna binti alikuja na mama mkwe wake mgonjwa anatakiwa kufanyiwa upasuaji na hana hela alilia yule binti sasa sijui katika hali kama hii mtu ukiwa huna hela inakuaje," alisema Nason.

Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Dk. Ally Senga, alisema taratibu za kujifungua kwa njia ya kawaida na upasuaji ni bure na hakuna fedha ambayo mtu anatakiwa kutozwa kwa ajili ya kupata huduma hizo.

Alisema kinachofanyika kama kuna upungufu wa vifaa tiba ndipo wanatakiwa kwenda kununua katika duka la dawa lililopo kwenye kituo hicho cha afya.

"Ni kweli duka la dawa lipo kwenye kituo chetu cha afya na maduka haya yalianzishwa baada ya kufuata muongozo wa serikali na duka hilo linatumika endapo tumepungukiwa dawa ndani ya hospitali ndipo tunawaelekeza waende huko," alisema Dk. Senga.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka aliagiza kufanyika uchunguzi juu ya tuhuma hizo ili kubaini mambo yanayotendeka katika kituo hicho cha afya cha Makambako na hatua zichukuliwe.

"Ni vizuri uchunguzi kwenye kituo kile cha afya ufanyike na ikiwezekana kama ni maafisa wetu pale wabadilishwe na wapelekwe maeneo mengine," alisema Mtaka.

Alisema serikali haiwezi kusema imepeleka miundo mbinu na vifaa tiba lakini kuna mambo ambayo siyo mazuri yanafanyika katika kituo cha afya na yanavumiliwa.

# TRA yatoa elimu mlango kwa mlango kwa wafanyabiashara

Na Elizabeth John, MAKAMBAKO

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Njombe, imelazimika kupita mlango kwa mlango katika maduka ya wafanyabiashara wa Halmashauri ya Mji wa Makambako kwa ajili ya kutoa elimu ya kodi na matumizi ya mashine za kielektroniki EFD.

Akizungumza na waandishi wa habari, Ofisa wa TRA, Daniel Shoo, alisema sababu ya kufanya operesheni hiyo ni baadhi ya wafanyabiashara kutoshiriki katika mikutano

"Tunatoa elimu mlango kwa mlango kwa sababu kuna wengine uwa hawaji kabisa kwenye mikutano, kwa hiyo tumeona tuwafate kwenye biashara ili kuwapata wote na kuwapa elimu ambayo ndiyo msingi kwenye biashara zao," alisema Shoo.

Ofisa Mwandamizi Elimu kwa MlipaKodi WA TRA, Isihaka Sharif, alisema eneo la Makambako ndiyo kitovu cha makusanyo kwa sababu ya kuwapo kwa walipakodi wengi na kwa kiwango kikubwa.

"Kwa hiyo pia lengo la kuwafuata katika sehemu zao za biashara ni moja ya mkakati wa kusogeza huduma kwa walipa kodi kwa maana tunaamini walipakodi wetu wanashughuli nyingi za kufanya," alisema Sharif.

Sharifu alisema wakati wanaendelea kutekeleza zoezi hilo wamebaini kuna changamoto kubwa ya matumizi ya mashine za kielektroniki (EFD).

Kutokana na hali hiyo, alisema bado kuna haja ya kutoa elimu zaidi katika matumizi ya MAshine zetu za kieletroniki yani EFD, pia wanafanyia kazi ombi la kurekebisha makadirio kutokana na wamesema mzunguuko wa biashara kutokuwa mzuri.

Mmoja wa wafanyabiashara,. Daines Sigala, aliipongeza TRAkwa kuwafuata na kuwapa elimu katika maduka yao, hivyo kuomba kutazamwa kwa jicho la huruma katika makadirio kwa sababu biashara imeporomoka.

"Kwenye makadirio tunachoomba yaani wakae viongozi, watusikilize wafanyabiashara maana yake sisi ni wamoja," alisema Sigala.





# Marekani yawanoa watumishi serikalini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZIARA za Rais Samia Suluhu Hassan katika nchi mbalimbali duniani zimeanza kuzaa matunda kwa utekelezaji baada ya watumishi na wataalamu wa serikali kuanza kupatiwa mafunzo ya matumizi sahihi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na mitandao ya kijamii.

Mkurugenzi wa Idara ya Mawasiliano Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Mzee Suleiman Mndewa aliyasema hayo jana wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo yaliyoandaliwa kwa ushirikiano wa serikali za Tanzania na Marekani.

Mndewa alisema Rais Samia alifanya ziara yake Marekani Aprili mwaka 2022, na Makamu wa Rais wa nchi hiyo Kamala Haris nchini, hivyo baadhi ya makubaliano yaliofikiwa yameanza kufanyiwa kazi kupitia sekta ya TEHAMA.

"Mafunzo haya yamewakutanisha watendaji wa Serikali zote mbili lengo likiwa ni kuwajengea uwezo wa matumizi sahihi ya TEHAMA na usalama mtandaoni," alisema.

Alisema matumizi ya mitandao kwa sasa hayana mipaka hivyo, kunahitajika umakini zaidi kwa watumiaji hali iliyopelekea Serikali ya Marekani kuanza kutoa mafunzo ya kujenga uwezo ili Tanzania nayo iwe salama katika hilo.

Mkurugenzi wa Usalama na TEHAMA Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari nchini, Steven Wangwe, alisema Serikali imeingia makubaliano ya ushirikiano na Marekani juu ya usalama mtandao, matumizi ya 5G na teknolojia zinazochipukia ili kulinda taarifa binafsi za watu.

Wangwe, alisema mafunzo hayo yanajumuisha uimarishaji wa miundombinu ya TEHAMA ili kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa mawasiliano.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Emmanuel Mkilia, alisema mafunzo hayo yatasaidia kwenda sambamba na teknolojia zinazoibuka na kuendelea kusimamia ulinzi wa taarifa binafsi za wateja.

Mkurugenzi Miradi wa Mpango wa Mashirikiano baina ya Serikali ya Marekani na Tanzania katika TEHAMA, William Garvison, alisema kuna changamoto katika usalama wa mtandao, hivyo utekelezaji wa ushirikiano huo utasaidia kukabiliana nazo.

# Salmin, Karume kupewa tuzo SUZA

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIKA Maadhimisho ya Miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kimeandaa tuzo maalumu kuwatambua viongozi na wataalamu waliozaa fikra ya kuanzishwa kwa chuo hicho.

Makamu Mkuu wa SUZA, Prof. Muhammed Makame Haji, alitangaza mpango huo jana ofisini kwake wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya chuo hicho kuelekea katika maadhimisho hayo.

Profesa Haji alisema tuzo hizo atakabidhiwa Rais Mstaafu wa Zanzibar, Dk. Salmin Amour Juma kutokana na mchango wake wa kutoa fikra za kuanzisha chuo chini ya sheria ya Baraza la Wawakilishi Na. 8 ya mwaka 1999.

Alisema Rais mstaafu, Dk. Amani Abeid Karume, atakabidhiwa tuzo kutokana na mchango wake wa kuanzishwa SUZA na kuwa mkuu wake wa kwanza. Prof. Haji alisema wengine watakaokabidhiwa tuzo hizo wakati wa maadhimisho hayo ambayo kilele chake hufanyika kila mwaka Januari 12 ni Haroun Ali Suleiman, Omar Ramadhan Mapuri, Dk. Abdulhamid Yahya Mzee na Dk. Saleh Idrisa Muhammed ambaye ni mwenyekiti wa kamati tendaji ya kuanzishwa SUZA.

Alisema SUZA imeandaa maonyesho ya uvumbuzi na tafiti yatakayofanyika Januari, mwakani na kuzindua Kigoda cha Karume kwenye kumbukizi ya miaka 52 ya kifo cha Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Abeid Amani Karume.

Akizungumzia kuhusu malengo ya chuo kwa mwaka wa fedha 2023/24, alisema kitaendelea kufanya mapitio ya mitaala ya programu ya stashahada ya elimu ya michezo na za kozi za elimu.

Malengo mengine ni kuandaa kozi za umahiri kwa usalama wa mitandao, kukarabati majengo ya utawala, kutoa kozi ya kompyuta, sayansi, maktaba, ujenzi wa nyumba za wataalamu na uchapishaji wa kitabu cha zungumza kiswahili hatua ya tatu na majarida.

Prof. Haji alitaja malengo mengine kuwa ni kutengeneza miongozo ya maabara za baiolojia, fizikia na kununua vifaa vya maabara.

Alisema tangu kuanzishwa kwa chuo hicho miaka 22 iliyopita kimepata mafanikio kwa kutengeneza wasomi na wabunifu wa ndani na nje ya nchi, kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaaluma.




Mkuu wa Wilaya ya Mjini Zanzibar, Rashid Simai Msaraka akiongea kwenye kikao na wandishi wa habari kuhusu suala la maegesho. Kushoto ni Mkurugenzi wa Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji mkongwe Zanzibar, Ali Said. **PICHA: MARTIN KABEAMBA**

# Dk. Mwinyi awamwagia sifa Skauti

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amekisifu Chama cha Skauti Tanzania kuwa kinafanya mambo makubwa katika jamii na kundi kubwa la vijana nchini.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla wakati wa ufunguzi wa mkutano mkuu wa chama hicho uliofanyika Chuo cha Utalii Maruhubi Zanzibar.

Alisema Skauti kinafanya kazi kubwa ya kuwajengea uwezo vijana kujitambua, kuwa na maadili mema na kuwakuza kizalendo ili kutengeneza taifa ambalo litaendelea kuwa na viongozi bora watakaosukuma mbele maendeleo.

Dk. Mwinyi, alisema viongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) zinaridhishwa na chama hicho pekee ambacho ni tofauti na asasi nyingine nchini kwa kulea vijana kwa kuzingatia misingi, kanuni na taratibu kupitia elimu isiyo rasmi inayozingatia tunu za kizalendo na maadili yanayoendana na taifa.

Alikitaka chama hicho kuendelea kuwasimamia vijana kwa kuwapatia elimu ya matumizi sahihi ya mitandao ya kijamiii kwa kujielimisha ili kukuza uelewano vinginevyo watashindwa kufikia malengo katika maisha yao ya baadaye.

Dk. Mwinyi aliiagiza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kuhakikisha shule na vyuo vinakuwa na Skauti na walimu wenye mafunzo bora katika maeneo yao.

Aliwataka viongozi wa Skauti kuzingatia sera ya usalama dhidi ya unyanyasaji na kuhakikisha vipengele vitakavyoingizwa katika katiba ya chama hicho vinaendana na matakwa ya agizo la Mkutano Mkuu wa Skauti Duniani uliofanyika mwaka 2021.

Rais wa Skauti Tanzania ambaye pia ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, alisema miongoni mwa taasisi muhimu nchini ni chama hicho kwa kuwa kinafanya kazi ya kuwalea vijana katika malezi bora, kuwaweka pamoja kufanya maamuzi na kuwafundisha uzalendo wa kulitumikia taifa lao.

Mkenda, alisema mkutano huo utatoa fursa ya kufanya mchakato wa upatikanaji wa katiba ambayo ndio muhimili mkuu wa chama hicho itakayosaidia kutatua changamoto zinazowakabili na kusimamia malengo ya maendeleo ya Skauti Tanzania.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar ambaye pia ni makamo wa Rais wa Skauti Tanzania, Lela Mohamed Mussa, alisema uamuzi wa kufanyika mkutano huo Zanzibar ni kuwasaidia viongozi wakuu wa nchi kuwaandaa vijana kuwa viongozi bora kwa baadaye.

Alisema faida ya uwepo wa Skauti nchini inaonekana kwani vijana wanaopitia katika chama hicho kulelewa katika maadili mema, kuwasaidia katika jamii na ujenzi wa taifa.

Mkuu wa Skauti Tanzania, Rashid Mchata, alisema chama hicho ni hazina kubwa ambayo ni chimbuko kuu la viongozi wengi wenye uzalendo na nchi yao.

alisema licha ya mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya Skauti, bado kinakabiliwa uhaba wa maeneo ya kuweka kambi kwa ajili ya kuwapatia mafunzo wanachama wao na ofisi za ngazi za mikoa na wilaya.

# HABARIPICHANI



Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk akisalimiana na Balozi wa Kuwait nchini, Mubarak Mohammed baada ya kuwasili katika Ubalozi huo Jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kusaini kitabu cha maombolezo kufuatia kifo cha Amir wa Kuwait, Sheikh Nawaf al-Ahmad Al-Sabah kilichotekea Desemba 16 mwaka huu.



Mkurugenzi wa Kituo cha watoto wenye uhitaji maalum cha Salt Special Centre kilichopo Mbezi Msakuzi, Rebecca Lebi, akionyesha bidhaa mbalimbali zinazotengenezwa na kituo hicho Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**



Kazi ya ujenzi wa barabara za mabasi ya mwendokasi ikiendelea katika eneo la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Wananchi wakipita jirani na sehemu ya kuhifadhia taka huku ikionekana kujaa, katika soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana.**PICHA: MIRAJI MSALA**



Kamanda kikosi cha Usalama Barabarani wilaya ya Muheza Tanga, Leonard Bandola akikagua leseni na vyeti vya udereva kwa madereva wanaoendesha vyombo vya moto juzi katika stendi kuu ya mabasi wilayani Muheza. **PICHA: STEVEN WILIAM**



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba (katikati) akimkabidhi funguo ya gari jipya la Idara ya Afya Muheza, Katibu Tawala Wilaya ya Muheza Mohamed Mfaki (kushoto) juzi katika hafla iliyofanyika ofisi ya mkuu wa mkoa wa Tanga. Watatu kushoto Mwenyekiti wa Halmashauri ya Muheza, Erasto Mhina na kulia ni Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Muheza Jumaa Mhina. **PICHA: STEVEN WILIAM**

# Israel, Hamas waendelea kutwangana Khan Younis

**GAZA,** PALESTINA

MJI wa Khan Younis, ulioko kusini mwa Gaza, umekuwa kitovu cha mapigano makali ya mitaani kati ya vikosi vya Israel na wanamgambo wa hamas.

Shirika la habari la Safa lenye uhusiano na Hamas liliripoti kuhusu mapigano hayo ikiambatana na mashambulizi ya anga ya Israel katika eneo la Ma'an.


Juzi usiku, msemaji wa Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF) Daniel Hagari, alisema vikosi vimeongeza na kuimarisha mashambuzi ndani ya Khan Younis.

"Tuliongeza kikosi kizima na vikosi vya ziada vya uhandisi kwenye operesheni katika eneo hilo ili kuboresha shughuli zetu katika eneo hilo," alisema Hagari.

Wakati huo huo, mkuu wa kundi la wapiganaji wa Hamas, Ismail Haniyeh, aliwasili jana nchini Misri na kuibua taarifa ya kuwepo kwa ishara ya mazungumzo.

Nchi za Misri na Qatar, zilisaidia kufikia makubaliano ya usitishwaji wa vita yaliyodumu kwa muda wa wiki moja na kushuhudia mateka kadhaa wa Israel na wafungwa wa Kipalestina wakiachiliwa huru.

Rais wa Israel Isaac Herzog, alisema nchi yake iko tayari kusitisha mapigano kwa ajili ya kutoa nafasi ya misaada ya kibinadamu eneo la Gaza na kuwezesha kuachiliwa kwa mateka wengine. **BBC**



Mgombea kiti cha urais nchini DRC, Moise Katumbi akipiga kura yake katika mji wa Lubumbashi jana. **PICHA: AFP**

# Uchaguzi DRC kuamua nani atakuwa rais

## •Katumbi, Fayulu walalamikia vifaa kuchelewa

RAIA wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC),jana wamepiga kura kuwachagua viongozi wa nafasi mbalimbali akiwamo rais, wabunge na viongozi wa serikali za mitaa.

Mpaka jana mchana wapiga kura waliojitokeza katika vituo vya kupigia kura zaidi ya 175,000 vilivyoko maeneo mbalimbali na vingi viko katika miji mikubwa ya Kinshasa na Lubumbashi.

Hata hivyo zoezi hilo lilichelewa kuanza katika vituo vingi huku maafisa wa tume wakifanya juhudi ya kuhakikisha watu wanapiga kura kikamilifu.

Ilielezwa idadi ndogo ya watu ilijitokeza katika vituo vingi lakini ilitarajiwa kuongezeka kadri muda ulivyosonga.

Mmoja wa waangalizi wa uchaguzi huo, Teresa Masele alisema upigaji kura ulianza kwa kuchelewa hatua ambayo huenda ikawakatisha tamaa wapiga kura waliojitokeza mapema katika baadhi ya vituo.

Hata hivyo, tume ya Uchaguzi ya DRC (CENI) ilisema wapiga kura wote waliojitokeza katika vituo, wataruhusiwa kushiriki zoezi hilo kama watakuwa wamejiandikisha.

Rais Felix Tshisekedi ambaye anawania muhula wa pili alipiga kura katika kituo kilichoko mjini Kinshasa.

Hata hivyo, mgombea wa kiti cha urais, Martin Fayulu, alisema uchaguzi huo umetawaliwa na vurugu maeneo ya vijijini.

Fayulu ambaye alipiga kura katika mkoa wa Gombe alikiri upigaji kura katika jiji hilo la Kinshasa unaendelea vizuri tofauti katika maeneo mengi ya vijijini.

"Nina watu wangu wanaozunguka nchi nzima na hakuna kituo kilicho tayari," alisema Fayulu.

Mgombea huyo wa chama cha ECiDé alitishia kukataa matokeo ya uchaguzi ikiwa raia hawataweza kupiga kura.

Mpinzani mkuu wa Rais Tshesekedi, Moise Katumbi alipiga kura majira ya saa tano katika mji wa Lubumbashi.

Baada ya kupiga kura, katumbi alisema ana uhakika wa kushinda uchaguzi na hakuna mtu anayeogopa lolote.

Mgombea huyo wa chama cha Ensemble pour la République, Moïse Katumbi, ambaye pia alikuwa Gavana wa jimbo la Katanga alilakiwa na maelfu ya wafuasi katika moja ya vituo vya kupigia kura mjini humo.

"Hatuogopi chochote kabisa. Tutashinda chaguzi hizi," alisema na kushangiliwa.

Alionya akisema "Lazima tufuatilie kura hadi mwisho. Lazima tuhesabu kituo cha kupigia kura kimoja hadi kingine, matokeo pekee ambayo tutakubali ni yale yatakayoonyesha katika kila kituo cha kupigia kura,"

Katumbi aliungana na wagombea wengine wa upinzani kwa kuelezea dosari zilizojitokeza na kushutumu uandaaji mbovu wa uchaguzi huo.

Hata hivyo, serikali ya DRC ilisema hakuna mtandao utakaozimwa wakati wote wa uchaguzi.

Hatua hiyo inatokana na watu kuwa na hofu ya kuzimwa kwa mitandao ya kijamii wakati wa uchaguzi.

"Hapana, hatutazima mtandao kwa sababu hatuko katika hali ya vita au uasi wa wananchi," alisema Waziri wa Mambo ya Ndani Peter Kazadi.

Aidha alionya kuwa wale wanaopanga kuvuruga mchakato wa uchaguzi watakamatwa.

Wakati huo huo, mamlaka ya usafiri wa anga ilitangaza kufunga mipaka ya nchi kavu na baharini kwa saa 24 kwa ajili ya kufanyika kwa uchaguzi huo mkuu.

Kulingana na Kurugenzi Kuu ya Uhamiaji, mipaka ilifungwa kuanzia Jumatano asubuhi hadi saa 11:59 jioni kwa saa za ndani ya nchi hiyo.

Anga ya Congo pia ilifunga safari zote za ndani ambazo hazijaidhinishwa, lakini safari za ndege za kimataifa ziliendelea kama kawaida.

Wapiga kura milioni 44 wamejiandikisha kwa ajili ya kushiriki uchaguzi mkuu.

Uchaguzi huo unaweza kutatanishwa na hali ya ukosefu wa usalama katika sehemu za Mashariki ya nchi hiyo na changamoto za vifaa vya elektroniki vya upigaji kura.

Mafanikio ya uchaguzi huo yataimarisha utulivu nchini humo na kuhakikisha raslimali za madini yananufaisha watu.

Rais Félix Tshisekedi ambaye anawania muhula wa pili, nafasi yake inatishiwa na wapinzani wake mkuu Moïse Katumbi na Martin Fayulu.

Wapiga kura pia wamechagua wabunge, magavana wa mkoa na viongozi wa manispaa ambao kwa jumla wapo wagombea 100,000.

**WANAOISHI NJE**

Raia kadhaa wa Kongo wanaoishi nchini Burundi waliruhusiwa kuvuka mpaka wa Kavimvira kwa ajili ya kushiriki uchaguzi mkuu.

Ubalozi wa DRC wa nchini Burundi ulitangaza kwamba unatoa vibali maalumu vya usalama bila malipo na kwa Wakongo wanaoishi nchini humo kwa ajili ya kwenda kupiga kura.

Balozi Willy Mulamba Mabika, alisema lengo ni kuwezesha kuvuka mpaka na usalama wa Wakongo waliokwenda Uvira kushiriki zoezi hilo muhimu.

Alibainisha kwamba sharti pekee ni kila aliyepatiwa kibali hicho lazima awe na kadi ya mpiga kura iliyotolewa mwaka wa 2023.

# JKT TANZANIA YAFUNGUKA ILIPOKWAMA, KUSAKA KIPA

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa JKT Tanzania, Malale Hamsini, amesema timu yake inapoteza mechi mbalimbali za Ligi Kuu Bara kutokana na makipa wake kufungwa mabao ya kizembe, hivyo analazimika kuingia sokoni kusaka nyota wapya watakaoongeza nguvu katika kikosi chake.

Malale alisema anaamini ujio wa makipa wapya utasaidia kuwapa changamoto magolikipa waliopo na hivyo kuisaidia timu kupata matokeo mazuri.

Kocha huyo alisema mara kwa mara timu yake imepoteza mechi za Ligi Kuu Bara kwa kufungwa mabao mepesi kutokana na makipa wake kufanya makosa ambayo yanazuilika.

„Ninatarajia kuingia sokoni katika dirisha dogo la usajili kusaka wachezaji wengine, pamoja na mambo mengine nitashusha kipa mwingine kwa ajili ya kuleta changamoto," alisema Malale.

Aliongeza katika mechi dhidi ya Azam FC kulikuwa na makosa ambayo yalisabisha waruhusu aina fulani ya mabao, lakini hali hiyo ilijirudia Jumatatu iliyopita walipocheza dhidi ya Coastal Union, na kufungwa bao 1-0.

„Tumefungwa goli jepesi, langoni kipa wetu anashindwa kuisaidia timu, kazi kubwa ya mwalimu ni kuwaelekeza wachezaji jinsi ya kutengeneza nafasi, lakini kuingiza mpira ndani ya wavu ni ya mchezaji mwenyewe, utaona tumetengeneza nafasi nyingi, lakini mtu yeye na kipa au na wavu anashindwa kufunga, halafu sisi tunafungwa bao rahisi vile, „ alisema kocha huyo.

Tayari Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), limeshafungua dirisha dogo la usajili na litafungwa rasmi Januari 15, mwakani na kalenda hiyo inazihusu timu zote za zinazoshiriki Ligi Kuu Bara, Ligi ya Championship, First League na Ligi Kuu Wanawake ambayo ilianza kwenye viwanja mbalimbali hapo jana.

JKT Tanzania inashika nafasi ya tisa katika msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 16 baada ya kucheza michezo 14.




Wachezaji wa Timu ya Walemavu wakifanya mazoezi ili kujiimarisha kwenye viwanja vya JKM Park jijini, Dar es Salaam jana.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

# Yanga Princess kibaruani Dodoma

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga Princess, Charles Haalubono, amesema kikosi chake kipo imara na tayari kuvuna alama tatu muhimu katika mchezo wa Ligi Kuu ya Wanawake dhidi ya Baobab Queens utakaochezwa leo kwenye Uwnaja wa Jamhuri jijini, Dodoma.

Yanga Princess ilimaliza katika nafasi ya tatu katika michuano ya Ngao ya Jamii baada ya kuifunga Fountain Gate Princess wakati Simba Queens ilibeba taji hilo la kwanza na JKT Queens ikimaliza katika nafasi ya pili.

Akizungumza na gazeti hili, Haalubono, alisema amekiandaa vizuri kikosi chake kuelekea mchezo huo ambao anaamini utakuwa na ushindani kwa sababu kila upande unahitaji pointi tatu.

Kocha huyo alisema hii ni mara yake ya kwanza kufundisha Tanzania lakini anaimani katika soka hakuna ugeni na kikosi chake kimejipanga kuhakikisha wanafanya vizuri katika mchezo huo wa ugenini.

„Tutacheza kwa tahadhari kubwa, tunaenda kupambana kusaka ushindi, hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu kila mmoja wetu amejiandaa vizuri, tutacheza kwa kuwaheshimu wapinzani. Utakuwa mchezo mzuri wa kimbinu na kiufundi," alisema Haalubono.

Aliongeza ameimarisha safu yake ya ushambuliaji ambayo ilikosa namba tisa wa asili na kushindwa kufanya vizuri katika michuano ya Ngao ya Jamii kwa sababu ya baadhi ya nyota wake wapya walichelewa kujiunga na kambi ya timu hiyo.

JKT Queens ndio mabingwa watetezi wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania ambayo inadhaminiwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti.

# Ushindani, ukongwe Mapinduzi Cup 2024

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KAMATI ya Mashindano ya Kombe la Mapinduzi Zanzibar imesema inatarajia kuona ushindani mkubwa katika michuano ijayo itakayochezwa kuanzia Desemba 28 hadi Januari 13, mwakani.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Mbarouk Othman, alisema jumla ya timu 12 zilizopangwa katika makundi matatu zitashiriki michuano hiyo.

„Tunatarajia kushuhudia mashindano yenye ushindani na ubora mkubwa, tunawaahidi kila kitu kitakwenda vizuri, maandalizi yako kwenye hatua za mwisho," alisema Othman.

Alitaja Kundi A litakuwa na mabingwa watetezi, Mlandege FC, Azam FC , Chipukizi, URA (Uganda) wakati Kundi B linaundwa na Simba, Singida Fountain Gate, APR (Rwanda) na Jamhuri ya Kisiwani Pemba.

Kundi C katika michuano hiyo inayofanyika kila mwaka na itakayochezwa kwenye viwanja viwili vya Uwanja wa Amaan na Gombani litakuwa na Yanga, Bandari (Kenya), KVZ (Unguja) na Vital'O ya Burundi .

## Extra Bongo sasa kujinadi Morogoro

**Na Sabato Kasika**

BENDI ya Extra Bongo inatarajia kufanya ziara maalumu ya kujitambulisha na kutoa burudani katika kipindi hiki cha Sikukuu ya Krismasi na mwaka mpya, imeelezwa.

Kiongozi wa bendi hiyo, Rogert Hegga, aliliambia gazeti hili, kila kitu kinakwenda vizuri na wanamuziki wake wanatarajia kuwapata burudani ya kiwango cha juu mashabiki wao.

„Ratiba yetu inaanzia Desemba 22, mwaka huu (kesho), tutakuwa kwenye Ukumbi wa Meridian ulioko Kinondoni halafu Desemba 24, tutakuwa King Dom Juice Round iliyoko eneo la Mlimani City," alisema Hegga.

Aliongeza siku ya Krismasi bendi hiyo inayotamba na kibao chake cha Penalti ya Mwisho watakuwa kwenye Ukumbi wa Tabata Hotel na siku inayofuata watafanya onyesho lao lingine katika ukumbi wa Babylon Pub ulioko Kilosa mkoani, Morogoro.

„Hiyo itakuwa ni mara ya kwanza kwa bendi yetu kutoka nje ya Dar es Salaam tangu ilipozinduliwa rasmi Desemba 2, mwaka huu, hivyo ni fursa kwetu kutambulisha ujio mpya wa Extra mikoani," Hegga alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ICARDI ANUKIA MADRID
REAL Madrid inakaribia kufanya hatua ya kushtukiza kumsajili mshambuliaji wa Argentina, Mauro Icardi, mwenye umri wa miaka 30 kutoka katika klabu ya Uturuki ya Galatasaray. **(Marca)**

### DORTMUND YAMTAKA REGUILON
KLABU ya Borussia Dortmund inavutiwa na beki wa Tottenham Hotspur, Mhispania Sergio Reguilon, mwenye umri wa miaka 27, ambaye anaichezea Manchester United kwa mkopo. Reguilon ana kipengele cha kumaliza mkopo wake katika mkataba wake. **(Bild)**

### IVAN AGOMBEWA ENGLAND
KLABU ya Brentford imezitahadharisha Arsenal na Chelsea zitalazimika kulipa ada ‚inayostahili' ikiwa zinataka kumsajili mshambuliaji wa England, Ivan Toney, mwenye umri wa miaka 27. **(Talksport)**

### ILING-JUNIOR SOKONI RASMI
KLABU za Tottenham Hotspur, Aston Villa na Brighton zimefanya mawasiliano na Juventus kumhusu winga, Samuel Iling-Junior, mwenye umri wa miaka 20, ingawa bado hakuna ofa yoyote iliyotolewa. **(Tuttomercatoweb)**

### SANCHO ATAJWA LEIPZIG
RB Leipzig imeonyesha nia ya kumsajili winga wa Manchester United, Jadon Sancho, mwenye umri wa miaka 23, lakini kumudu mshahara wa mchezaji huyo wa kimataifa wa England inaweza kuwa tatizo kwa klabu hiyo ya Ujerumani. **(Bild)**

### UNITED KUTOSAJILI JANUARI
WAKATI Jadon Sancho anaweza kuondoka, Manchester United haitarajii kufanya usajili wowote mkubwa ifikapo Januari, Mkurugenzi wa Soka, John Murtough, amewaambia mashabiki wa klabu hiyo. **(The Athletic)**

### PALHINHA MAMBO BADO
KIUNGO wa kati wa Fulham na Ureno, Joao Palhinha, mwenye umri wa miaka 28, hatalengwa tena na Liverpool katika dirisha na Januari. Klabu nyingine kubwa zinamtaka ingawa Bayern Munich inamchukulia kuwa ni gharama kubwa kwao. **(Sky Sport Germany)**

### NEWCASTLE KUBANA MILEY
KLABU ya Newcastle United imeanza mazungumzo na kiungo wa kati wa England, Lewis Miley, mwenye umri wa miaka 17, kuhusu kusaini mkataba wa muda mrefu atakapofikisha miaka 18 hapo baadaye msimu huu. **(Telegraph)**

### GORE KWA MKOPO
PRESTON North End imeonyesha nia ya kumsajili kwa mkopo kiungo wa kati wa Manchester United, Dan Gore, mwenye umri wa miaka 19 katika muda wake uliobakia. **(Manchester evening News)**

### BARDGHJI AGOMBEWA EPL
KLABU ya Copenhagen iko tayari kumuuza winga wa Sweden, Roony Bardghji, mwenye umri wa miaka 18 anayelengwa na Chelsea, Manchester United na Tottenham Hotspur katika dirisha la Januari. **(90 min)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# NEYMAR NJE FAINALI COPA AMÉRICA 2024

**Nyota huyo sasa atarejea dimbani Agosti, mwakani baada ya...**

**SAO PAULO, Brazil**

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Neymar, atakosa michuano ya Copa América 2024 itakayochezwa nchini Marekani kwa sababu ya jeraha baya la goti alilopata Oktoba, mwaka huu, daktari wa timu hiyo, Rodrigo Lasmar, amesema.

Nyota huyo wa Al Hilal mwenye umri wa miaka 31, alipasuka mishipa ya nyonga na ya goti lake la kushoto wakati nchi yake ilipopoteza mechi ya kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Uruguay Oktoba 17, mwaka huu kabla ya kufanyiwa upasuaji wiki mbili baadaye.

Michuano ya Copa America itafanyika kuanzia Juni 20, mwakani na fainali yake itachezwa Julai 14, 2024.

„Ni mapema mno," alisema Lasmar akiiambia Rede 98 ya Brazil.

„Hakuna haja ya kuruka hatua za kupona mapema na kuchukua hatari zisizo za lazima. Matarajio yetu atakuwa tayari kurejea mwanzoni mwa msimu wa 2024 huko Ulaya, ambayo ni Agosti.

„Tunahitaji kuwa na subira. Kuzungumza kuhusu kurudi kabla ya miezi tisa ni mapema, hii ni dhana ya kimataifa kwa ajili ya kupona upasuaji wa mishipa ya goti. Ni muhimu sana kuheshimu muda wa kibaiolojia, muda ambao mwili huchukua muda kujijenga upya.

„Ikiwa tutafuata hatua hizo na baada ya kupona kwa muda mrefu, matarajio anaweza kuumia kwa kiwango cha juu."

Neymar ndiye mfungaji bora wa muda wote wa Brazil akiwa na mabao 79 katika mechi 129 alizocheza.

Brazil imepangwa Kundi D katika michuano ya Copa América pamoja na Colombia, Paraguay na mshindi wa mchujo kati ya Costa Rica na Honduras.


Mapema Jumanne, ilitangazwa Brazil itacheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Mexico itakayofanyika Juni 8, mwaka huu.

Ni mara ya pili kwa michuano ya Copa América kuandaliwa na Marekani baada ya mwaka 2016 ambapo ilikuwa ikitimiza miaka 100 tangu kuanzishwa kwake, huku timu sita kutoka Concacaf zikiungana na 10 kutoka Amerika Kusini.

Baada ya miaka sita kupita akiwa na Paris Saint-Germain, Neymar alijiunga na Al Hilal kwenye Ligi Kuu ya Saudi Arabia iliyotumia euro milioni 90 kama ada yake.

Aliichezea klabu mara tano pekee kabla ya kuumia, akifunga bao moja.

# GUARDIOLA AONYA FAINALI KLABU BINGWA YA DUNIA



**JEDDAH, Saudi Arabia**

PEP Guardiola amewaambia wachezaji wake wa Manchester City watapata fursa ya „mara moja katika maisha“ kushinda taji la Klabu Bingwa ya Dunia katika fainali zitakazochezwa hapo kesho.

City walitinga fainali kwa ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Urawa Red Diamonds ya Japan katika mechi ya hatua ya nusu fainali iliyofanyika juzi.

Klabu hiyo ya Ligi Kuu England sasa itacheza fainali dhidi ya  mabingwa wa Amerika Kusini, Fluminense.

City wanapewa nafasi kubwa ya kushinda taji lao la tano mwaka wa 2023, lakini Guardiola amekionya kikosi chake kulichukulia poa kombe hilo.

„Tutaenda kula chakula cha jioni pamoja, tutengeneze mazingira ambayo kila mtu anajua jinsi mchezo huo ni muhimu kwa klabu,“ alisema Guardiola.

„Kama nilivyosema, ili kucheza fainali hii lazima ufanye mambo ya ajabu, ili kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya. Mara tu tukiwa hapa, ni kombe ambalo unacheza mara moja katika maisha yako.

„Kuwa hapa ni jambo la kushangaza kwetu, hatuchukulii kawaida, tunajua labda hatutarudi tena.“

Wakati huo huo, City wameiambia FIFA nyota wake, Erling Haaland na Kevin De Bruyne hawatashiriki katika fainali hiyo.

Wachezaji wote wawili wamesafiri hadi Saudi Arabia na Jumatatu De Bruyne alifanya mazoezi na kikosi hicho kwa mara ya kwanza baada ya kukosa miezi mitatu kutokana na jeraha la misuli ya paja.

Haaland hajacheza tangu walipofungwa 1-0 na Aston Villa Desemba 5, mwaka huu na bado hajarejea mazoezini.

Baada ya kucheza na Fluminense, City wataivaa Everton katika mechi ya Ligi Kuu England itakayochezwa Desemba 27, mwaka huu kwenye Uwanja wa Goodson Park.

# Mourinho ataka Arsenal ibebe EPL

**ROME, Italia**

JOSE Mourinho amekiri angependa kuona Arsenal ikishinda taji la Ligi Kuu England (EPL), msimu huu, lakini Manchester City na Liverpool ndizo pekee ndio washindani wa kweli.

Washikabunduki hao wanaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu England baada ya mechi 17, wakiwa wamekaa pointi moja mbele ya Liverpool na Aston Villa, huku mabingwa watetezi City wakipitwa pointi tano nyuma.

Akizungumza kwenye kipindi cha John Obi Mikel kwenye The Obi One Podcast, Kocha huyo wa Roma, Mourinho, aliulizwa mawazo yake kuhusu nani atashinda taji la mwaka huu la England.

„Naweza kusema City asilimia 51 na Liverpool asilimia 49,“ alijibu Mourinho.

Alipoulizwa mara ya kwanza kuhusu matumaini ya Arsenal, Mourinho alijibu tu: „Nah!“

„Ushindani tofauti, ningependa washinde,“ aliongeza.

„Ni kweli, Chelsea haitashinda. Haina swali. Bila shaka, Manchester United haitashinda pia. Kwa hiyo ni kati ya hizi tatu , ingawa mimi ningependa Arsenal washinde.

Wakati akiwa Kocha wa Tottenham Hotspur, Mourinho alizungumza vyema kuhusu kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, akiwataka washikabunduki hao kusimama naye wakati wa kipindi kigumu.

„Nataka kumpa neno zuri Mikel kwa sababu alitupa mchezo mgumu sana,“ alisema Mourinho kuhusu Arteta baada ya Spurs kuishinda Arsenal 2-0 Desemba, mwaka 2020.

## Juve yadhamiria kumsajili Phillips

**TURIN, Italia**

JUVENTUS imezungumza na Manchester City kuhusu Kalvin Phillips wakati wanaangalia kuongeza kiungo wa kati ifikapo Januari, lakini wanatafuta chaguzi kadhaa katika hatua hii, vyanzo vimeiambia 90min.

City wameweka wazi kwa Phillips anaweza kuondoka Januari iwe kwa uhamisho wa kudumu au kwa mkopo.

90min ilifichua mapema mwaka huu, Phillips alikuwa akijitolea hadi Krismasi kujaribu kumshawishi, Pep Guardiola, alikuwa na jukumu la kuichezea City.

Hata hivyo, hilo halijatimia na mchezaji huyo wa zamani wa Leeds United sasa yuko tayari kuondoka.

Kwa muda mrefu Juventus wamekuwa wakimtaka nyota huyo wa kimataifa wa England.

Wanatazamia kuleta kiungo wa kati Januari, na wamezungumza na City kuhusu maelezo ya dili la Phillips.

Timu hiyo ya Serie A ingependelea kumchukua Phillips kwa mkopo wa awali na City wako tayari kufanya hivyo.

City ingependa kifungu cha lazima cha ununuzi katika mpango huo, lakini wako wazi kwa chaguo ambalo litakuwa na vichochezi vya kuifanya iwe ya kudumu.

Huenda Juve inakiasi kidogo cha fedha na Januari kama klabu nyingi, ingawa uwezekano wa kusimamishwa kwa Paul Pogba kunaweza kusaidia.

Zaidi ya hayo, Juve wanaangalia malengo mengine na Mkurugenzi wa Michezo, Cristiano Giuntoli, amekuwa akifanya kazi yake juu ya chaguzi nyingi.



## HABARI MICHEZO

# JULIO AMWAGIA PONGEZI BENCHIKHA, ONANA CAF

**Na Adam Fungamwango**

NYOTA na kocha wa zamani wa Simba, Jamhuri Kihwelo 'Julio' amemwagia sifa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Abdelhak Benchikha, kufuatia ushindi wa mabao 2-0 walioupata katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Wydad ya Morocco iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi.

Ushindi huo umeifanya Simba ifikishe pointi tano na kukaa katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Kundi B nyuma ya vinara ASEC Mimosas yenye pointi 10.

Julio alisema mbinu zilizofundishwa na Benchikha ndio zilizoamua mechi hiyo ambayo matokeo yake yamefufua matumaini ya Simba kusonga mbele katika michuano hiyo ya kimataifa.

Beki huyo wa zamani wa Wekundu wa Msimbazi pia alisifu kiwango kilichoonyeshwa na winga raia wa Cameroom, Essomba Onana, ambaye alipachika mabao yote mawili katika mechi hiyo.

„Kwa muda mfupi tu ameibadilisha Simba na kama atapata muda mrefu itakuwa timu ya kutisha zaidi, sio Tanzania, bali Afrika nzima, kuifunga Wydad Casablanca si jambo jepesi, ndugu zangu hizi timu za Waarabu siyo za mchezo mchezo, ni timu ngumu na nzuri ambazo mara nyingi zinachukua hivi vikombe vya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho," alisema mchezaji huyo wa zamani wa Simba aliyeitumikia klabu hiyo kati ya mwaka 1980 hadi katikati ya 1990.

Aliongeza anaamini Simba itarejea katika ubora wake na kuwa tishio kwa sababu ya ujio wa kocha huyo mkongwe hapa barani Afrika.

Kuhusu Onana, Julio alisema anadhani Benchikha amembadilisha tofauti kocha aliyepita ambaye alimwacha afanye anavyotaka

„Tatizo la Onana ni kujinufaisha yeye na nadhani kocha wa zamani alikuwa hamkemei, huyu aliyekuja naona kama anamkemea na unaona amebadilika kwa vitu anavyovifanya, si mchezaji mbaya, ni mzuri," alisema Julio.

Naye mchezaji wa zamani wa timu hiyo, Sharaf Eldin Shiboub, alisema kocha Benchika ndiyo nyota wa mchezo katika mechi hiyo kwa sababu alichanga karata zake vizuri na alizuia kila kitu kipindi cha pili.

„Pongezi kwa wachezaji wote, walikuwa na viwango bora, lakini pongezi zangu kubwa na za dhati nizipeleke kwa Kocha Mkuu (Benchika), aliicheza mechi vizuri sana mechi hii, hasa kipindi cha pili, alizuia kila kitu cha Wydad Casablanca," alisema kiungo huyo ambaye kwa sasa anaichezea APR ya Rwanda na alikuja nchini kwa ajili ya kuangalia mechi hiyo.

Alimtaja Onana ni mchezaji mzuri na mwenye kipaji, lakini akaongeza mabao aliyofunga yametokana na ushirikiano wa wachezaji wote.

## Dodoma Jiji yatarajia makubwa

**Na Saada Akida**

UJIO wa Kocha Mkuu mpya wa Dodoma Jiji FC, Francis Baraza, unatarajiwa kukiongezea nguvu kikosi cha timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji, Kassim Lyogope, alisema wanaamini Baraza ataisaidia timu hiyo kufikia malengo na muda wa kuijenga na kuiimarisha timu bado upo.

Lyogope alisema pia yeye binafsi anafurahi kuungana na Mkenya huyo kwa sababu anaamini atamwongezea mbinu za kufundisha kutokana na uzoefu ambao kocha huyo anao.

„Tutazaliwa upya, Dodoma Jiji itaimarika na itabadilika, tusubirie mambo mazuri baada ya ujio wa Baraza, anaijua Ligi Kuu ya Tanzania, anawajua wachezaji wengi wa hapa nchini, kikubwa ni tuongeze ushirikiano katika kutimiza majukumu yetu," alisema kocha huyo.

Aliongeza wameshaanza kufanyia kazi makosa yaliyojitokeza katika mechi zilizopita na wataingia kwenye mzunguko wa pili wakiwa na nguvu mpya.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Dodoma Jiji yenye pointi 18 iko kwenye nafasi ya saba baada ya kucheza michezo 13 wakati vinara wa ligi hiyo ni Azam FC yenye pointi 28 na imeshuka dimbani mara 12.



Mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis (kulia), akijiandaa kumtoka nyota wa Wydad katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. Simba ilishinda mabao 2-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Job awataka wachezaji Mtibwa kuzinduka

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa Yanga, Dickson Job, amewataka wachezaji wa Mtibwa Sugar kupambana na kuipigania timu hiyo inayoburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ili kuepuka janga la kushuka daraja.

Ikiwa nyumbani kwenye Uwanja wa Manungu Complex ulioko Turiani, Morogoro juzi Mtibwa Sugar iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mashujaa FC, lakini matokeo hayo hayajawanasua kutoka mkiani.

Job aliliambia gazeti hili Mtibwa Sugar ni moja ya timu kubwa nchini na haitakuwa vyema kuiona klabu yake hiyo ya zamani ikienda kushiriki Ligi ya Championship msimu ujao.

Beki huyo ambaye hakucheza mechi ya Jumamosi iliyopita dhidi ya timu yake hiyo ya zamani, aliwataka wachezaji wa Mtibwa Sugar 'kuamka', kujituma na ili kusaka matokeo mazuri yanayowanusuru na balaa hilo.

„Mtibwa Sugar ni timu kubwa ambayo imetoa wachezaji wakubwa na wenye heshima nchi hii. Kikubwa ninawaomba waendelee kupambana, wachezaji wote wajitoe, Mtibwa imetoa nyota wengi, achana na sisi wa miaka ya karibuni.

Kuna wachezaji waliofanya mambo makubwa waliwahi kupitia hapa, haitakuwa vyema kwa macho yetu tukiiona inashuka, hatutajisikia vizuri," alisema Job.

Kabla ya kupata ushindi huo wa juzi, Jumamosi iliyopita Mtibwa Sugar ilipata kichapo cha mabao 4-1 dhidi ya Yanga, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

„Naamini wanapitiwa na wakati mbaya tu, angalia katika mechi yetu wamecheza vizuri tu, ni matatizo madogo madogo sana yanawasumbua, watarudi kwenye nafasi waliyoizoea," alisema Job ambaye alijiunga na Yanga mwaka 2021 akitokea Mtibwa Sugar.

Mtibwa Sugar ambayo imekuwa na misimu mibaya mitatu mfululizo, imejikusanyia pointi nane katika michezo 14 ambayo imecheza msimu huu.



# Michezo

Alhamisi Desemba 21, 2023
Nipashe




Neymar nje fainali Copa América 2024 UKURASA 21

# YANGA SC YATAKATA CAF

## ••• Yatanguliza mguu mmoja robo fainali baada ya kuichapa Medeama...

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya kwanza Yanga imefanikiwa kupata ushindi katika mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika tangu mfumo huo ulipoanzishwa mwaka 1998, baada ya kuichapa Medeama kutoka Ghana mabao 3-0 na kurejesha matumaini ya kutinga hatua ya robo fainali.

Yalikuwa ni mabao ya raia wa Ivory Coast, Pacome Zouzoua na Watanzania, Bakari Mwamnyeto na Mudathir Yahya, ambayo yaliifanya timu hiyo kufikisha pointi tano na kukwea hadi nafasi ya pili katika msimamo wa Kundi D, huku mechi nyingine ilitakiwa kuchezwa jana kati ya CR Belouizad ya Algeria dhidi ya Al Ahly ilipigwa kalenda kutokana Wamisri hao kwenda Saudi Arabia kushiriki michuano ya Klabu Bingwa ya Dunia.

Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara wamebakisha mechi mbili ili kujua mustakabali wao katika kundi hilo dhidi ya CR Belouizad itakayochezwa Februari 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na ya mwisho watakapowafuata Al Ahly jijini, Cairo Machi Mosi, mwakani.

Iliwachukua Medeama sekunde 21 tu tangu mpira kuanza kufika katika lango la Yanga baada ya krosi ya Manuel Mantey, kuunganishwa kwa kichwa na Derick Fordjour, lakini kilikosa shabaha na kutoka nje.

Dakika ya tisa, Nickson Kibabage, ambaye alikuwa akimwendesha 'puta' beki wa kulia wa Medeama, Emmanel Godjoe, alipomzidi mbio na kuingia ndani ya eneo la hatari, lakini kabla hajaamua nini afanye, mpira ulifagiliwa na beki wa kati, Fatawu Hamidu na kuwa kona.




Wachezaji wa Yanga wakishangilia baada ya kupata bao la kwanza katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Medeama iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

Medeama nusura wajifunge dakika ya 12, baada ya kona iliyopigwa na Mudathir Yahya ilipowachanganya mabeki, lakini wakati mashabiki wa Yanga wakiwa wamesimama kutaka kushangilia bao, kipa, Felix Kyei, akaruka kama mkizi na kuutoa mpira ukawa kona.

Pacome alikosa bao dakika ya 20 alipopiga shuti la mbali lililopanguliwa na Kyei na kuwa kona ambayo pia ilileta kizaazaa, Bakari Mwamnyeto akiruka juu na kuupiga kichwa akiwa peke yake, lakini akakosa shabaha, ukatoka nje.

Baada ya kosa kosa nyingi, hatimaye Yanga ilifanikiwa kupata bao dakika ya 33 lililowekwa wavuni na Pacome, ni la tatu kwa mfungaji huyo katika michuano hiyo, moja akilifunga dhidi ya timu hiyo hiyo ya Medeama na lingine dhidi ya Al Ahly.

Ni aina ile ile ya mabao ambayo amekuwa akifunga katika michuano hiyo, kwani aliupata mpira akiwa mbele kidogo ya katikati ya uwanja na akaanza kuwafungasha tela wachezaji wa timu pinzani, akaingia kwenye eneo la hatari na kujitengenezea nafasi, kabla ya kupiga shuti kali lililomshinda Kyei kudala na kutinga kimiani.

Kama wangetulia, Yanga wangemaliza kazi dakika 45 za mwanzo wakiwa na idadi kubwa ya mabao, kwani licha ya kutawala karibuni kipindi chote hicho, lakini walikosa magoli mengi ya wazi kupitia kwa Musonda, Maxi Nzengeli, na Pacome pia.

Dakika ya 52, Medeama ilifanikuwa kupata penalti iliyosababishwa na Mwamnyeto aliyemwangusha, Foffi Babil, ndani ya eneo la hatari, lakini mchezaji aliyefunga penalti kwenye mchezo wa kwanza nchini Ghana, Jonathan Siwah, safari hii alikosa kutokana na kipa wa Yanga, Djigui Diarra, kupangua.

Ilionekana kama baada ya kukosa mkwaju huo wa penalti ni kama Medeama walichanganyikiwa na kupoteza hali ya kujiamini, haikushangaza walipopachikwa bao dakika ya 61 lililofungwa na Mwamnyeto.

Kama vile haitoshi, dakika tano baadaye, Mudathir alipachika bao la tatu lililotokana na makosa ya wachezaji wa Medeama ambao walianzisha mpira nyuma na kipa wao, lakini ulinaswa na Yao Kouassi, aliyempelekea Stephane Aziz Ki, naye bila uchoyo alimwekea sehemu nzuri mfungaji akaukwamisha wavuni kirahisi.

## Benchikha: Bado hatujamaliza kazi

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Wydad kutoka Morocco juzi, Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, amewapongeza wachezaji wake kwa kuonyesha kiwango kizuri na kuongeza bado hawajamaliza kazi.

Simba ambayo imefikisha pointi tano na kupaa hadi katika nafasi ya pili kwenye Kundi B, imebakiza mechi mbili ambapo itaifuata ASEC Mimosas huko Ivory Coast na itamaliza hatua hiyo kwa kuikaribisha kwenye Uwanja wa Mkapa, Jwaneng Galaxy kutoka Botswana.

Benchikha aliliambia gazeti hili jana, Simba inahitaji kuendelea kufanya vyema katika mechi zake nyingine mbili zilizobakia ili kufikia malengo ya kusonga mbele katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika yanayoendelea.

Kocha huyo alisema anaimani kubwa na kikosi chake na anaamini kinauwezo wa kufanya vizuri ili kucheza hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Alisema mechi hiyo ilikuwa ya ushindani na kila timu ilicheza vizuri lakini amewapongeza wachezaji wake kwa kufuata maelekezo aliyowapa kwenye uwanja wa mazoezi.

„Wachezaji wamefanya kazi nzuri, tumefanya mashambulizi na kufunga lakini hatukuruhusu bao, kipindi cha pili Wydad walitawala eneo letu, walifanya mashambulizi na kubadilisha mfumo kwa kuongeza mabeki.

Nafasi ya kwenda robo fainali ipo wazi, kazi iliyopo kwetu ni kujiandaa na michezo miwili iliyosalia ambayo tunahitaji ushindi ili kujihakikishia safari yetu ya kucheza robo fainali," alisema Benchikha.

Aliongeza baada ya mechi hiyo wanarejea kwenye uwanja wa mazoezi kwa ajili ya kufanyia kazi makosa yaliyojitokeza ili kujiandaa na mchezo ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC utakaochezwa kesho.

Naye mfungaji wa mabao yote katika mechi hiyo ya juzi, Essomba Onana, alisema Benchikha amempa morali na ari ya kujituma kufanya vizuri kutokana na kumwamini.

"Huu ushindi ni wetu wote, niwapongeze wachezaji wenzangu, tumepambana kusaka ushindi, lakini pia mashabiki wa Simba wanatakiwa kuwa wakweli, tunapokuwa katika wakati mgumu na furaha tuungane pamoja," alisema Onana.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >